Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project

Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Nafasi Ya Ahlulbayt (as)

Author(s):

Allamah Syed Murtadha Askari [3]

Publisher(s):

Al Itrah Foundation [4]

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la: "The role of Ahlul Bait (as) in Preserving the teaching of Islam" Tarjuma ya Mulla Asghaar M. M. Jaffer kutoka lugha ya Kiarabu. Sisi tumekiita: "Nafasi ya Ahlul Bayt katika kuhifadhi mafubdisho ya Kiislamu."

Translator(s):

Ramadhani Kanju Shemahimbo [5]

Category:

The 12 Imams [6]
Hadith Collections [7]

Topic Tags:

Historia [8]
Wakristo [9]
Wayahudi [10]
Hadithi [11]

Person Tags:

Mtume Muhammad (s.a.w) [12]
Ahlul Bayt (as) [13]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la: **"The role of Ahlul Bait (as) in Preserving the teaching of Islam"** Tarjuma ya **Mulla Asghaar M. M. Jaffer** kutoka lugha ya Kiarabu. Sisi tumekiita: **"Nafasi ya Ahlul Bayt katika kuhifadhi mafub- disho ya Kiislamu."**

Mwandishi wa kitabu hiki amelishughulikia sana suala la *'tawhid'*. Suala hili limezua mjadala mkali sana miongoni mwa wanachuoni wa Kiislamu, wengine wakimhusisha Mwenyezi Mungu na viungo na makazi na wengine wakiwa wanaikataa dhana hiyo, kila upande ukitoa hoja na dalili zake. upande mmoja ni wa wanachuoni wa Madhehebu ya Sunni ambao wanaunga mkono dhana hii, na upande mwingine ni wa wanachuoni wa Kishia ambao wanapinga dhana hiyo.

Mwandishi wa kitabu hiki (**Allamah Syed Murtadha Askari,** mwanazuoni wa Kishia'h) amelishughulikia suala hili kwa kulinganisha hoja za pande zote mbili kwa kutumia vitabu vyao vya *tawhid* na vya hadith, na akahitimisha kwa kuonesha pasina shaka yoyote kwamba Mwenyezi Mungu yu mbali na hayo wanayo mhusisha nayo.

Sisi tunamuachia msomaji asome kwa makini na utulivu, na uwamuzi utakuwa ni wake; bali matumaini yetu ni kwamba ataelekea kule kwenye haki, bila ya kujali haki hiyo iko kwa nani.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya 'Al-Itrah Foundation' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia

Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu, **Ramadhani Kanju Shemahimbo** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19071 Dar-es-Salaam.

Marhum Mulla Asghar ameacha alama isiyosahaulika katika Jumuiya nzima ya Shi'a katika zama hizi.

Mtu mwenye kipaji cha ubora huu, na athari kama hii, anachipukia mara moja tu katika maisha. Kama mubaligh adhimu, aliwasilisha kwa ufasaha kabisa mafundisho ya Ahlul Bayt (a.s.) kwa watu kwa jumla. Akithibitishwa na wanazuoni wa wakati wake, umaizi wake wa kina katika masuala ya Fiqh, theolojia, falsafa, teosofia (imani kwamba wanadamu wanaweza kumfahamu Mungu na kuwasiliana Naye kwa kutulia na elimu ya kina) na vile vile masuala ya nyakati hizi, yeye alikuwa maarufu. Kama muelimishaji kwa kiwango cha hali ya juu kabisa, uwezo wake wa kujulisha na kuelimisha wanafunzi wake juu ya fikra za Kiislamu kwa kweli ulikuwa unataalimisha sana. Kwa kupitia fikra zake, maandishi yenye kuchochea na hotuba zenye msukumo, vichwa au akili nyingi zimefanywa zianzishe tafakari, na maisha ya watu wengi yamebadilishwa. Athari zake juu ya jamii yetu ilikuwa kama ya ajabu sana na ambayo imekuwa ya kusaidia sana katika kubadilisha mifano (ya maisha).

Ninatumaini kwamba mfululiza huu wa vitabu wenye ukumbusho, vinavyozingatia maadhimisho ya miaka 25 ya Jumuiya yetu ya Kimataifa – *World Federation* – utaendelea kunururisha mafundisho ya Ahlul–Bayt (A.S.) kwa ulimwengu kwa jumla kupitia maneno ya mwanazuoni huyu mashuhuri. Kwa kuunga mkono Mfuko wa Kumbukumbu wa Mulla Asghar (*Mulla Asghar Memorial Fund*), ambao, miongoni mwa miradi ya kielimu, umefanya mfululizo huu wa machapisho kuwezekana, utasaidia kuhakikisha kwamba mapenzi yake juu ya kueneza mafundisho ya Ahlul– Bayt (A.S.) yanaendelea baada yake. Kwa pamoja, tunaweza kuleta ukweli kwenye zile ndoto nyingi alizokuwa nazo na kusaidia World Federation kuendelea katika njia ya huduma ambayo aliieneza chini ya uongozi wake wenye haiba kubwa. Ninawaombeni kumkumbuka Mulla Saheb kwa kumsomea *Suratul–Fatihah*

Hasnain Walji
Raisi, World Federation, KSI Muslim Communities.

Kuhusu Mwandishi

Allamah Syed Murtadha Askari

Allamah Syed Murtadha Askari ni mwanazuoni wa Shia'h anayetambulika, ambaye vitabu vyake katika historia ya Kiislamu, masomo yanayowiana ya madhehebu mbalimbali ndani ya jamii ya Uislamu na falsafa, vimeacha alama isiyofutika.

Kwenye kutambulika heshima yake kuna vitabu vikubwa kama "Abdullah ibn Saba," "Masahaba wa Mtume (s.a..w.w.) 150 wa bandia," na kile "Sifa bainifu za kawaida za madhehebu mbili (za Kiislamu)." Baadhi ya uchambuzi wa awali na uchunguzi wa kisayansi katika nyanja ya historia ya Kiislamu umevunja zile fikra na mawazo yaliyokuwa yamekubalika hadi sasa, na kusababisha makelele yasiyo na kifani, ambayo hayajawahi kutokea miongoni mwa washikilia elimu ya vitabuni wasiobadilika na wenye

imani kamili ya dunia ya Kiislamu.

Kama mwanaharakati wa kisiasa, Allamah anafahamika kwa maoni yake thabiti na mapambano juu ya kuhuisha Uislamu. Wengi wa marafiki zake na washirika wake wameuawa kishahidi na utawala katili wa Iraqi. Allamah yuko juu sana miongoni mwa wanazuoni wakubwa wanaoweza kusimama kutokana na makumbusho ya nyuma ya mapambano makali dhidi ya uasi wa kujitokeza kwa Wa–Ba'th. Yeye ni mzungumzaji mwenye mvuto na muongeaji mcheshi; na hata katika umri wa zaidi ya miaka themanini, haonyeshi dalili yoyote ya kudhoofika kwa raghba!

Mwenyezi Mungu amdumishe zaidi!

Utangulizi : Athari Ya Imani Za Kikristo Na Kiyahudi Katika Uislamu

Imani za kikristo na kiyahudi, hususan utamaduni wa kiyahudi ulienea miongoni mwa Waislamu katika njia mbili: kwanza kabisa, kupitia juhudi za wakristo na wayahudi wenyewe, na pili kupitia kwa Waislamu fulani.

Hebu tuzichunguze njia hizi mbili kwa kinaganaga:

Kuenea kwa imani za Kikristo na Kiyahudi miongoni mwa Waislamu kupitia juhudi za makusudi kabisa za Wakristo na Wayahudi.

Huko nyuma, tumeelezea nafasi ya wanazuoni wa Kikristo na Kiyahudi katika kuzua hadithi. Tunajua kwamba pale Makhalifa walipokataa kuruhusu uenezaji wa hadithi za Mtume (s.a.w.w.), kwa hisani sana wao waliwaruhusu wanazuoni wa Kikristo na Wayahudi ambao walikuwa wameingia katika Uislamu ili kueneza fikra zao wenyewe miongoni mwa Waislamu. Mathalan, Tamim Darii, aliyekuwa mtawa wa Kikristo kabla ya kuukubali Uislamu, aliruhusiwa rasmi na Khalifa Umar kuhutubia Waislamu siku za Ijumaa, kabla ya hotuba ya Swala ya Jama'a, ndani hasa ya Msikiti mkuu wa Mtume (s.a.w.w.). Katika zama za Uthman, aliruhusiwa rasmi kufanya hivyo mara mbili kwa wiki.

Vivyo hivyo, Ka'b al–Ahbar (ambaye jina lake la kwanza lilikuwa ni Mati') alikuwa ni kuhani aliyefahamika vizuri kabla yeye kuukubali Uislamu. Alijulikana kama Ka'b al–Habr au Ka'b al–Ahbar, kwani Habr kwa Kiarabu ina maana ya mtakatifu, mtu mwenye elimu. Katika siku za Khalifa Umar, Ka'b al–Ahbar alipandishwa kwenye cheo cha Msimamizi wa Baraza, na Uthman vile vile aliendelea kumlea yeye. Waislamu walimwendea katika mas'ala ya kanuni na ufafanuzi wa Qur'ani Tukufu.1

Ka'b alijaribu kiasi alivyoweza katika kueneza imani zilizochimbukia kutoka kwenye masimulizi

yaliyopotoshwa ya Taurati, na dhana nyingine za Kiyahudi, miongoni mwa Waislamu. Baadhi ya watu wa wakati huo huo ambao waliwafuata Ahlul-Bayt (A.S.) walikuwa wanatambua juu ya mbinu zake za kichochezi, kama inavyoshuhudiwa katika kadhia ifuatayo:

Tabari katika kitabu chake cha historia anasimulia:

"Ibn Abbas aliambiwa: Ka'b anasema kwamba katika Siku ya Kiyama, jua na mwezi vitakuja kuletwa kama madume ya ng'ombe mawili yaliyochanganyikiwa na kutupwa ndani ya Jahannam."

Alipoyasikia haya, Ibn Abbas alikasirika sana, na akajibu kwa ukali mara tatu:

"Ka'b ni muongo! Ka'b ni muongo! Ka'b ni muongo! Hii ni fikra ya Kiyahudi, na Ka'b anataka kuiingiza katika Uislamu. Mwenyezi Mungu yuko Huru kutokana na vitu wanavyomhusisha navyo. Yeye kamwe haviadhibu vile vinavyomtii. Hujamsikia Mwenyezi Mungu akisema ndani ya Qur'ani Tukufu kamba:

وَسَخَّرَ لَكُمُ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَائِبَيْنِ ۖ وَسَخَّرَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ {33}

"Na akakutiishieni jua na mwezi, vifanyavyo kazi (***vikifuata njia zao***) ***mfululizo.'"*** (***Ibrahim; 14: 33***)

Ibn Abbas akasema: "Hii ***'Daibain'*** iliyotumika katika Ayah hii inaonye- sha utii wa wakati wote kwa Mwenyezi Mungu."

Kisha akaendelea:

"Yeye atawezaje kuyaadhibu haya maumbo mawili ya ki-mbinguni ambayo Yeye Mwenyewe anayasifia kwa utiifu wao? Mwenyezi Mungu Amlaani mwanazuoni huyu wa Kiyahudi na elimu yake! Ni ufidhuli usio na aibu kiasi gani huu wa kuhusisha uongo kwa Mwenyezi Mungu, na kutia hatia kwa viumbe viwili hivi vitiifu!"

Baada ya kuyasema haya, Ibn Abbas akarudia mara tatu kusema: **"Sisi sote ni wa Allah, na Kwake Yeye tutarejea."**

Halafu Ibn Abbas akaendelea kusimulia kile ambacho Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hasa alichokisema kuhusu jua na mwezi. Mtume alisema:

"Mwenyezi Mungu ameumba vyanzo viwili vya mwanga. Kile ambacho Yeye alikiita jua kilikuwa kama ardhi, baina ya sehemu za mawio na machweo. Na kwamba kile alichokiamuru kuwa bila mng'aro kwa nyakati fulani, Yeye alikiita mwezi na akakifanya kuwa kidogo zaidi kuliko lile jua. Na vyote huonekana kuwa kama vidogo kutokana na urefu wao katika anga na umbali wao kutoka ardhini."2

Uchunguzi Ulioegemea Juu Ya Hadith Hizo Mbili

Kutoka kwenye Hadith hizi mbili, ambazo ni, ile moja kutoka kwa Ka'b na nyingine kutoka kwa Ibn Abbas, tunaona kwamba:

1. Ibn Abbas alikanusha na kukataa yale ambayo Ka'b aliyahusisha na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akanukuu kutoka kwenye Qur'ani Tukufu:

"Na akakutiishieni jua na mwezi, vifanyavyo kazi (vikifuata njia zao) mfululizo……."

Akitoa hoja kwamba juhudi yote hiyo ni sawa na utii kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hakuwaadhibu wale au vile vinavyomtii Yeye.

2. Katika kukataa zaidi tabia ya Ka'b ya kufuata mkondo wa yaliyotangulia, Ibn Abbas alithibitisha kwamba jua na mwezi yalikuwa ni maumbo makubwa mawili ya kimbinguni kama ardhi, na alitafuta kuungwa mkono na Hadith ya Mtume (s.a.w.w.), ambayo imesema:

"Na vyote huonekana kuwa kama vidogo kutokana na urefu wao katika anga na umbali wao kutoka ardhini."

Ni dhahiri, haya yalikuwa ndio maamuzi bora kabisa ambayo Ibn Abbas aliyoweza kuyafanya kutoka kwenye Hadith. Hata hivyo, katika zama hizi, tunao uwezo wa kupata mahitimisho zaidi kutoka kwenye Hadith, yaani:

i. Kutajwa kwa sehemu ya mawio na machweo kwa ajili ya jua kuhusiana na ardhi, kunatoa kidokezo kuhusu mizingo na mzunguko wa maumbo ya kimbinguni.

ii. Vile vile kunaashiria kwamba maumbile hayo yanapaswa kuwa ya mviringo (matufe) ili kuwa na sehemu mbalimbali za kutua na kuchomoza. Hili lisingewezekana kama yangekuwa ya ubapa.

iii. Ni wazi vile vile kutokana na namna Ibn Abbas alivyoijadili ile Hadithi iliyosimuliwa na Ka'b kwamba yeye hakuelekea kuukubali uwezo wa kisheria wa Ka'b.

Kwa hiyo, Hadith zote kama hizo, ambazo zina mwonjo wa imani za Kiyahudi na zinahusishwa bila matata kwa Ibn Abbas kwamba amezisikia kutoka kwa Ka'b, hazina msingi na sio za kweli. Hizi zilibuniwa katika wakati wa siku za utawala wa Bani Abbas kwa sababu Bani Abbas walimuamini sana mhenga wao Ibn Abbas. Watu walitengeneza hadithi kwa jina la Ibn Abbas ili kupata umaarufu katika mabaraza ya Bani Abbas. Ulikuja kuwa ni mtindo kuhusisha hadithi za uongo kwa Ibn Abbas, ambazo badala yake ziliunda sehemu kubwa sana ya propaganda ya Kiyahudi na Kikristo.

Ibn Abbas alikuwa na uwezo wa kupata maamuzi fulani kutoka kwenye Hadith za Mtume (s.a.w.w.). Tunao uwezo wa kufanya nyongeza kwenye maamuzi hayo, tukiegemeza uchunguzi wetu juu ya ukweli wa kielimu wa wakati huu. Inaelekea kabisa kwamba hapo baadaye, wakati elimu itakapokuwa imefanya

uchunguzi wa ziada, wanazuoni wanaweza kufanya mahitimisho mapya na ya maana zaidi kutoka kwenye Hadith. Lakini simulizi ya Ka'b ni upuuzi wa Kiyahudi, na inazidi kuwa bure zaidi kadiri muda unavyosonga mbele.

Baadaye katika mjadala huu, tutaonyesha taswira ya nafasi kubwa ya Ka'b, kuthibitisha jinsi alivyofanikiwa katika majaribio yake ya hatari.

Kwa masikitiko makubwa, Hadith hii kutoka kwa Ka'b kuhusiana na jua na mwezi kutokea Siku ya Kiyama kama mafahari wawili waliochanganyikiwa, ilipata njia ya kuingia kwenye vitabu vya Kiislamu kupitia kwa masahaba kama Abu Huraira na wengineo.

Haya yametokea licha ya makanusho ya hasira ya Ibn Abbas. Katika *Tafsiir* ya Ibn Kathiir na katika *Kanzul Ummal*, imesimuliwa kutoka kwa Abu Hurair kwamba:

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Katika Siku ya Kiyama, jua na mwezi vitakuwa katika moto wa Jahannam katika umbile la mafahari wa ng'ombe wawili waliochanganyikiwa."

Mtu mmoja akamuuliza: "Lakini ni kwa dhambi gani walizofanya hadi kustahili adhabu hiyo?"

Abu Huraira akajibu vikali: "Mimi ninakusimulieni ambacho Mtume (s.a.w.w.) amekisema, na wewe unaniuliza mimi namna ya dhambi zao?"

Katika Hadith nyingine dhaifu kutoka kwa Anas, Ibn Kathiir anasimulia yafuatayo:
"Jua na mwezi vitakuwa katika moto wa Jahannam kama madume ya ng'ombe mawili yaliyochanganyikiwa."

Maoni Yetu Juu Ya Haya Yaliyopita

Hadith hizi kutoka kwa Abu Huraira na Anas kwa kweli zinafanana, ni hiyo hiyo moja ambayo ilibuniwa na Ka'b al–Ahbar. Zimehusishwa kwa uwongo kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Kama tukiichunguza Ayah hii ya Qur'ani Tukufu na Hadith sahihi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), tunakuta kwamba haditi hii ya Ka'b ni uzushi wa mawazo yake mwenyewe, zilizoegemea kwenye fikra za Kiyahudi. Baada ya kuthibitisha kwamba hadithi hii kutoka kwa Ka'b imehusishwa kwa Mtume kwa visingizio vya uongo na kwa msaada wa Ibn Abbas aliyeishutumu kwamba ni utomaji maneno (yasiyokuwepo) wa Kiyahudi, hayabakii mashaka yoyote kwamba chanzo cha hadithi hii ni Ka'b al–Ahbar mwenyewe na wala sio hawa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Hatari hii ilikuwa imetambuliwa na masahaba wa mwanzoni wa Mtume (s.a.w.w.). Ibn Abbas alikuwa miongoni mwa wale wa kwanza kusimama kidete dhidi ya mashambulio ya muingilio wa Kiyahudi, na Imam Ali (a.s.) vilevile alimuonya Khalifa Umar kuhusu jambo hili.

Kwa vile Ka'b hakuwa miongoni mwa masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) hakuweza kuhusisha kiini cha

imani yake ya Kiyahudi kwa Mtume mwenyewe moja kwa moja. Njia ya kufaa sana kwake ilikuwa ni kuandaa njia ambayo ingezichukua hadithi hizo kwa kutumia majina ya masahaba fulani fulani kama Abu Huraira na wengineo.

Ingawa ile hadithi kutoka kwa Anas imethibitishwa kwamba ni dhaifu, hadithi nyingine kutoka kwa Abu Huraira juu ya suala hilo hilo ilichukuliwa kama ni sahihi, na kwa hiyo ikatoa nguvu kwenye uzushi wa Ka'b. Ilikuwa ni juhudi ya pamoja, za makusudi kabisa au vinginevyo, za wale wanazuoni wa Kikristo na Kiyahudi waliosilimu, na masahaba kadhaa na wale ambao walifuatia zama za masahaba.

Kuenea Kwa Imani Za Kikristo Na Kiyahudi Miongoni Mwa Waislamu Kupitia Kwa Waislamu Wenyewe

Ili kuifanya hoja yetu ieleweke vizuri zaidi, tunatoa mifano miwili ya masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na vile vile nukuu kutoka kwenye mojawapo ya *Tafsiir*.

(1) Abu Huraira, Mmoja Wa Masahaba Wa Mtume (S.A.W.W.):

Historia imerekodi majina matatu tofauti ya sahaba huyu mmoja. Hata hivyo, yeye ni maarufu sana kwa Kuniyat yake ya Abu Huraira. Yeye alitokana na kabila la Dus, ambalo lilichipukia kutoka Yemeni. Abu Huraira aliishi huko kwa miaka thelathini na aliwasili Madina baada ya vita vya Khaibar. Kwa mujibu wa Bukhari, Ibn Sa'd na wengineo, yeye alikuwa pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika ile miaka mitatu ya mwisho.

Lakini ukichukulia ule ukweli kwamba aliondoka kwenda Bahrain mnamo mwezi 8 Hijiria pamoja na jeshi lililoongozwa na Ala' Hadhrami, jumla ya siku zake pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ni dhahiri kwamba inakuwa ndogo zaidi.

Alikuwa akiishi pamoja na wale Waislamu masikini katika kishubaka cha jiwe kilichojulikana kama Suffah kilichokuwa kimekingama katika Msikiti wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Wakati Mu'awiyah alipomtuma yule muuaji muovu sana, Busr, ambaye alihusika na yale mauaji ya halaiki ya Waislamu thelathini elfu wasiokuwa na hatia, baina ya Syria na Yemeni, Abu Huraira aliteuliwa kuwa kama gavana wa Madina kwa baraka zake Busr.3 Halafu aliendelea kubakia na nafasi hiyo hiyo kwa muda fulani katika utawala wa Mu'awiyah.4

Hizi zilikuwa ndio siku za Abu Huraira ambazo alipata muda muafaka haswa wa kuzieneza hadithi zake. Baadhi ya masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walikuwa kwa kweli wanao ujuzi hasa katika sanaa ya kusoma na kuandika lakini kwa bahati mbaya, Abu Huraira alikuwa sio mmoja wao. Bukhari anamnukuu yeye akisema: Abdullah bin Amru Aas alikuwa anajua kuandika wakati mimi nilikuwa sijui." Miongoni mwa watu ambao kutoka kwao yeye alipata faida za hali ya juu sana alikuwa ni Ka'b al–Ahbar ambaye alitoa sifa zifuatazo kwa Abu Huraira:

“Kati ya watu ambao hawakuwa wamesoma Taurati na bado wakawa na ujuzi na kuifahamu vizuri sana, Abu Huraira alikuwa ndio mbora wao.”5

Hii ni kusema kwamba, mbali na yule rabi (kiongozi wa dini ya Kiyahudi) ambaye bila shaka alikuwa ameisoma Taurati, Abu Huraira kwa umaarufu aliwapita wengine wote katika ujuzi wa Taurati. Cha kufurahisha vya kutosha, Ibn Kathiir ndani ya *Tariikh* yake anatoa maoni hivi:

“Abu Huraira alikuwa mdanganyifu, akichanganya kwa ulaghai kile alichokisikia kutoka kwa Ka’b na kile ambacho alikisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), bila ya kuyapambanua moja kutokana na jingine.”

Anaendelea zaidi kusema kwamba: “Wafuasi na marafiki zetu wanazitupilia mbali baadhi ya hadithi za Abu Huraira.”

Na vile vile anasema: “Wao hawakuweza kukubali kila hadithi ambayo ilisimuliwa na Abu Huraira.”6

Kipengele kinachouma sana ni kwamba Abu Hurair bila haya na hofu anasimulia hadithi mbili zinazopingana kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Bukhari ndani ya *Kitab al-Tib* anasimulia yafuatayo kutoka kwa Abu Huraira:

“Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: ‘Maradhi hayaambukizi au kuenea.’ Kisha Mwarabu mmoja akasimama kuuliza: ‘Ewe Mtukufu Mtume, tunao ngamia wazuri sana katika jangwa. Lakini pale mmoja wao anapopatwa na ugonjwa wa vidonda, wengine nao vile vile huwa wanaambukizwa.’ Mtume (s.a.w.w.) akauliza: ‘Huyo ngamia wa kwanza aliambukizwa vipi?’”

Baada ya kunukuu hadithi hii, Bukhari anaendelea kusimulia hadithi nyingine:

“Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameagiza kwamba wale ambao wanaugua na wenye maradhi wasiwatembelee wale wenye afya njema.” Abu Salmah, ambaye ni binamu yake Abu Huraira akauliza: “Ewe Abu Huraira! Hivi wewe hukusimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuwa akiamini juu ya maambukizo?”

Katika kujibu, Abu Huraira alitoa matamshi fulani katika lugha ya Kihabeshi! Kisha yule binamu yake Abu Huraira akasimama kumtetea Abu Huraira kwa kusema:

“Sijawahi kamwe kumuona Abu Huraira akiwa msahaulifu isipokuwa kati ka tukio hili.”

Ni dhahiri kwamba, Abu Salma alikuwa akijaribu kuhalalisha ule upinganaji katika hadithi za Abu Huraira. Hata hivyo, msemo maarufu unasema hivi: *“Pale mtu anapokuwa kama Abu Huraira, huyo huelekea kusahau.”*

Abu Huraira Anakiri

Cha kushangaza ajabu ni kule kukubali kwa Abu Huraira mwenyewe kwamba amewahi kusimulia hadithi fulani fulani kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) bila ya kuwa amezisikia kutoka kwake.

Imam Ahmad Hanbal anasimulia tukio fulani ndani ya Musnad yake:

"..... na Abu Huraira alisimulia hadith na wasikilizaji wake wakauliza: "Hii inatoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au imetoka mfukoni mwako?" Abu Huraira akasema: "Hii moja makhsusi ni yangu mwenyewe kutoka mfukoni mwangu."

Bukhari analisimulia tukio hili kama ifuatavyo:

"Abu Huraira aliulizwa: 'Je hii uliisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?" Naye akajibu: "La hasha, hadithi hii ni yangu mwenyewe."

Katika hadithi nyingine iliyosimuliwa na Imam Ahmad Hanbal, tunayakuta haya:

"Abu Huraira alisimulia Hadith kana kwamba ameisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), lakini mwishowe alikiri kwamba ilikuwa ni yake mwenyewe kutoka mfukoni mwake."

(2) Abdullah Bin Amru Aas, Mtetezi Wa Hadithi Za Kiyahudi:

Abdullah bin Amru Aas (aliyefariki mnamo mwaka wa 65 Hijiria) anachukuliwa kama mmoja wa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kwa vile alikuwa amerithi hazina kubwa ya dhahabu ya Ki–Misri kutoka kwa baba yake, alijulikana kama mmoja wa matajiri wakubwa miongoni mwa masahaba. Yeye aliijua lugha ya Syria (*Suryani*), lugha asili ya Taurati.

Katika vita vya Yarmuk, yeye aliongoza jeshi la baba yake kama mshika bendera wake, na aliweza kuzitia mkononi shehena za ngamia wawili za vitabu vya Kiyahudi na Kikristo.7

Dhahabi anasema:

"Abdullah amesimulia kutoka kwa Watu wa Kitabu. Alivisoma vitabu vyao kwa mfululizo, na alionyesha upendeleo maalum juu ya vitabu hivyo."

Ibn Hajar katika *Sharhe* yake juu ya *Sahih Bukhari* anasema:

"Abdullah katika mapambano ya Damascus alipata shehena ya ngamia mmoja ya vitabu vya Kiyahudi na Kikristo kama ngawira ya kivita. Alivisoma kwa uangalifu sana na akazitegemeza hadithi zake juu ya vitabu hivyo. Kwa sababu ya hili, watu maarufu wa kundi la Tabi'in (waliofuata baada ya masahaba) walijizuia kusimulia kutoka kwake."

Katika Musnad ya Imam Ahmad Hanbal tunayakuta yafuatayo:

“Mtu mmoja alikuja kwa Abdullah na akasema: ‘Hebu niambie kile ulichokisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wala usinisimulie zile hadithi kutoka kwenye Taurati na Injili.”

Katika hadithi nyingine tunasoma haya:
“Abdullah aliambiwa: ‘Hebu niambie yale uliyoyasikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wala usinisimulie yale uliyoyapata kutoka kwenye ile shehena ya ngamia wa Yarmuk.”8

Wanazuoni wa Hadith wa Kiislamu wamezitenga Hadith hizo kama ni za kiyahudi (Israiliyyat) – kwa sababu ya asili yao kutoka kwenye Taurati na vyanzo vingine vya Kiyahudi.

Katika lundo la Hadith zilizotwaliwa na wale Waislamu ambao hawatokani na madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.), tunazikuta Hadith nyingi zinazozungumzia juu ya Mwenyezi Mungu kuwa na mwili. Hizi ni dhahiri kabisa kwamba zinatoka kwenye vyanzo vya Kiyahudi na mara kwa mara tunakuta kwamba zimesimuliwa kutoka kwa Ka’b al-Ahbar au Abu Huraira. Tutakuja kuzijadili hizi kwa kina hapo baadaye.

(3) Maqatil Ibn Sulayman Balkhi:

Yeye huyu alikuja kutoka Balkhi. Aliachiwa huru na kabila la Azd, na akat- waa kuniyat ya Abul Hasan. Katika kuishi kwake mjini Basra na Baghdad, alisimulia hadithi kadhaa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.), na alikubalika kama mmoja wa wanazuoni maarufu wa elimu za Qur’ani Tukufu na ile madhehebu kinyume na ya Ahlul-Bayt (a.s.).

Miongoni mwa vitabu vilivyotungwa na yeye ni:

Tafsir Kabir – ambacho nakala ya mwandiko wa mkono bado ipo nchini Misri.

Nawadir ya Tafsiri

Al-Ayat al-Mutashabihat

Al-Nasikh wal Mansukh

Al-Qiraat

Al-Ashbah wa al-Nazair fil Qur’an al-Karim

Al-Jawabat fil Qur’an

Ibn Khaldun, katika kitabu chake cha wasifu cha Maqatil, anasimulia kutoka kwa Ibn Habban kwamba:

“Alikuwa akikubali ufafanuzi wa Qur’ani Tukufu kutoka kwa Wayahudi na Wakristo ambao waliitafsiri kwa mujibu wa vitabu vyao wenyewe!”

Na halafu anaendelea tena:

“Maqatil alikuwa miongoni mwa wale waliohusisha sifa za kibinadamu na namna ya kufanana (analojia) kwa Mwenyezi Mungu, na zaidi ya hayo, yeye alikuwa anadanganya wakati alipokuwa akisimulia Hadith.”9

Khatib Baghdadi katika historia yake – Taarikh Baghdad anasema:

“Siku moja, Muhammad bin Said Kalbi (aliyefariki 146 Hijiria) alitokea kupita karibu na Maqatil na akamsikia yeye akisimulia baadhi ya Hadith fulani fulani, akizihusisha kwa Kalbi mwenyewe. Hivyo akasema: ‘Ewe Maqatil! Mimi ndiye Muhammad bin Said Kalbi, na kamwe sijasimulia hadithi hizo ambazo umezitaja hivi punde hapa!”

Maqatil akasema:

“Tunazipamba hadithi zetu kwa majina ya wasimuliaji mashuhuri.”
Maqatil alikuwa na maana kwamba aliambatanisha majina ya wasimuliaji mashuhuri kwenye uzushi wake mwenyewe ili kwamba upate kusadikika!

Muhammad bin Said Kalbi vile vile anasimuliwa kuwahi kusema kwamba:

“Maqatil amezihusisha kwangu kwa uongo hadith ambazo sijawahi kuzitamka, na yeye amezijumuisha katika Tafsir yake.”

Khatib Baghdadi ndani ya maelezo yake juu ya Maqatil anasimulia tukio lililosimuliwa na watu wawili:

“Tuliuliza kutoka kwa Maqatil kuhusu chanzo cha hadithi yake moja mahususi, naye akasema: ‘Mimi niliisikia kutoka kwa Dhahhak.’ Baada ya siku chache tulipomuuliza tena kuhusu hadithi ile ile, yeye akasema: ‘Niliisikia kutoka kwa Ata.’ Katika wakati mwingine aliihusisha kwa Isa.

Baada ya kulisimulia tukio hili, Khatib Baghdad anasema kwamba mtu mmoja alimuuliza Maqatil kama aliwahi kumuona kamwe huyo Dhahhak, ambaye amedai kuwahi kumsikia. ‘Hakika ndiyo!’ Akasema Maqatil. ‘Kulikuwa na mlango uliokuwa umefungwa kati yangu na yeye.’”

Baghdad anaelezea kwamba kwa ile “mlango uliofungwa,” Maqatil alimaanisha lile lango kuu la jiji la Madina, kwa vile Dhahhak aliishi Madina na yeye Maqatil hajawahi kufika huko Madina kamwe.

Ibn Khallikan anasema:

“Dhahhak bin Mazahim, ambaye kutoka kwake Maqatil alisimulia hadith, alifariki miaka minne kabla yeye Maqatil hajazaliwa, na alizikwa ndani ya uwanja wa makaburi huko Madina!”

Zaidi ya hayo, yeye anaongezea:

“Maqatil alisimulia kutoka kwa Mujahid bila hata ya kuwa amewahi kuku– tana naye!”

Khatiib Baghdad ameandika kisa kifupi cha kuvutia sana (kinachomhusu Maqatil). Yeye anasema:

“Mtu mmoja alimuuliza Maqatil: ‘Rafiki yangu alitaka kujua rangi ya yule mbwa wa *As’habul–Kahf*. Mimi sikuwa na jibu la kumpatia.”

Maqatil mara moja akajitolea kujibu. Yeye akasema:

“Mwambie mbwa huyo alikuwa na madoadoa. Hakuna mtu atakayekanusha hili!”

Anaendelea kusimulia kutoka kwa Mansur na Mahdi, wale wafalme wa ki– Bani Abbas kwamba Maqatil wakati mmoja alijitolea kutunga hadithi chache za uongo katika kumsifu mhenga wao Abbas, kama wao wangependa hivyo. Wote wawili walimkatalia.10

Kwa kupitia vitabu kadhaa ambavyo ndani yake picha ya haraka ya maisha ya Maqatil imeonyeshwa, tunakuta mifano mingi ya uzushi na udanganyifu. Kuhitimisha, yeye alikuwa ni wakili madhubuti wa ile dhana ya kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa na umbo la mwanadamu.

Yeye alijifunza tafsiri ya Qur’ani Tukufu kutoka kwa washauri wake wa Kiyahudi na Kikristo na akazinakili imani zao katika kitabu chake juu ya *Tafsir*. Licha ya haya, inashangaza kweli kweli kuona kwamba wanazuoni kutoka madhehebu kinyume na ile ya Ahlul–Bayt (A.S.) wamemimina sifa nyingi juu ya *Tafsir* yake.

Ibn Khalidun anasema:

“Katika elimu ya Tafsir, watu wote ni wanyenyekevu kwa Maqatil bin Sulayman ...!”

Mifano Ya Hadithi Zilizotengenezwa Na Maqatil, Katika Kuwaunga Mkono Makhalifa:11

Khatib Baghdad, katika kitabu chake kikubwa cha historia, Tarikh Baghdad, anasimulia kupitia nyororo inayoendelea ya wasimuliaji:

Maqatil amesema: “Dhahhak amenisimulia mimi kutoka kwa ibn Abbas kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alishauriwa na masahaba zake kumteua mrithi wa nafasi yake ili aweze kujulikana kwa watu, na kwamba watu watapeleka masuala yao kwake. ‘Hatujui ni nini kitakachotokea baada ya w e we kuondoka.’”

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akajibu:

“Kama ningeteua mtu ambaye angewaongozeni ninyi katika kumtii Mwenyezi Mungu, nanyi mkaacha kumtii yeye, basi mtakuwa mnapuuza maagizo yangu na yale ya Mwenyezi Mungu. Na kwa upande mwingine, kama mtu kama huyo aliyeteuliwa akawaelekezeni katika kufanya maovu na mkamtii, mtakuwa mmewekwa vyema Siku ya Kiyama kumtaja yeye kama mwenye uwezo wa kisheria. La hasha,

mimi sitafanya kamwe jambo kama hilo – ni afadhali mimi nikawaacheni kwenye uangalizi wa Mwenyezi Mungu!”

Tathmini Ya Hadith Hiyo Hapo Juu:

Hadith hii ilibuniwa na Maqatil ili kuwaunga mkono Makhalifa ambao walidai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuteua mrithi yeyote wa nafasi yake, na kwamba haki ya uteuzi kama huo ilikuwa mikononi mwa umma wa Kiislamu.

Inapendeza kuona kwamba Khatib ameinakili hadith hiyo hapo juu kwenye kitabu chake cha wasifu wa Maqatil kuthibitisha kutoaminika kwake na udanganyifu wake. Anahoji kama Maqatil alikuwa na ujasiri wa kusimulia kutoka kwa Dhahhak bila ya yeye kukutana naye kamwe. Dhahhak aliishi Madina, ambapo Maqatil hakuwahi kusafiri kutoka Khurasan kwenda Madina. Ukweli ni kwamba Dhahhak alifariki miaka minne kabla Maqatil hajazaliwa!

Baada ya mfano huo hapo juu wa upenyezaji wa Kiyahudi na Kikristo katika imani za Kiislamu, tunaona inafaa kunukuu visa viwili vifupi kutoka kwenye Taurati. Hivi vitasaidia sana kwenye tathmini ya imani zinazashikiliwa na madhehebu kinyume na ile ya Ahlul-Bayt (a.s.), hususan kuhusiana na Sifa za Mungu.

1. Kuumbwa Kwa Adam

Katika Kitabu kile cha Mwanzo, Mlango wa Kwanza, mstari wa 27, tunasoma kama ifuatavyo:
“Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu yeye alimuumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba,”

Hadithi hiyo inaendelea kusema kwamba Adam na Hawwa waliwekwa katika Bustani ya Adeni. Halafu Mungu “akawapotosha”:

“Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, usile: kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.**11** Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akawaambia: ‘Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.’

‘Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala,akam- pa na mumewe, naye akala.
Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi.

‘Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone. ‘Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, uko wapi?

‘Akasema: Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. Akasema, Ni nani aliyekwambia ya kuwa u uchi? Je! umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?’

‘Ndipo Adamu akaeleza yale ambayo yaliyotokea, hivyo Mungu akawaapiza Adamu, Hawwa na yule nyoka na akawalaani wao na vizazi vyao kwenye maisha ya kuhangaika, huzuni na kazi ngumu juu ya ardhi.

‘Bwana Mungu akasema, basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele. ‘….. Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Adeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima.”11

2. Shindano La Mieleka Kati Ya Yakobo (Yaqu– Ub) Na Mungu:

Usiku mmoja, Yakobo alipigana mieleka na Mungu hadi kukacha, lakini Mungu hakufaulu kumshinda Yakobo!

“Yakobo akakaa peke yake; na mtu mmoja akashindana naye mweleka hata alfajiri. Naye alipoona ya kuwa hamshindi….. akasema: ‘Niache, niende maana kumepambazuka.’ Akasema: ‘Sikuachi usiponibariki.’

‘Akasema: Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda… Na Yakobo akapaita mahali pale, Penueli, maana alisema, nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka.’”12

Maana Ya Visa Hivi Vifupi:

Kwa uwazi kabisa, Mungu wa Wayahudi ni wa kipuuzi na asiye makini. Analala na kama mwanadamu yeyote mbinafsi, anasema uongo na kudanganya!

Alimdanganya Adam pale alipomuonya asile kutoka kwenye ule mti kwa sababu ingeweza kumsababishia kifo; na alikuwa ni yule nyoka ndiye ambaye aliuondoa udanganyifu huo kutoka kwa Adam na akamlaghai yeye kula kutoka kwenye mti huo. Halafu Adam akawa kama mmoja wa miungu, anayeyajua mema na maovu, akijitambua kwamba alikuwa yuko uchi, alijificha mbele ya Mungu! Wote watatu, yule nyoka, Adam na Hawwa walilaaniwa na kuteseka na kazi ngumu juu ya ardhi!

Kwa mujibu wa Taurati, Mungu ana kiwiliwili; anatembea kutoka sehemu moja kwenda nyingine, na anapigana mieleka na hawezi kumuona mtu anayejificha kutoka machoni Kwake!
Hizo ndizo hadithi za dhihaka za Taurati.

Athari Ya Jumla Ya Taurati

Tunaweza tukawagawanya watu walioathiriwa na upuuzi kama huo katika makundi tofauti yafuatayo:

1. Watu ambao walishtushwa kuona kwamba vitabu vilivyodhaniwa kwamba viliteremshwa kwa Mitume wakubwa kama Musa na Isa, amani juu yao wote, vilikuwa na makosa mengi sana na simulizi potovu na zisizo za kimaadili. Na kwa matokeo ya kupoteza imani kwao, walizitelekeza dini zote zilizofunuliwa na wakageuka kuwa wapenda anasa za dunia katika mwelekeo wao.

2. Kuna kundi jingine ambalo ni imara katika njia ya kidini waliyoichagua, licha ya kuangukia kuwa waathiriwa wa dhana hizi zisizo na maana.

Hawa wako katika vikundi vitatu:

A. Wayahudi

Wao wanahusika na upotoshaji na utomaji wa maneno ndani ya Taurati, na upotoshaji huo unaonekana katika mtazamo wao wa maisha na mwelekeo wao wa kitamaduni. Wanawafundisha watoto wao kufuata mbinu zile zile za ulaghai, kusema uongo na udanganyifu. Wanajiona wao wenyewe kuwa ndio wana wa Israeli, yule ambaye alipigana mieleka na Mungu na akashinda. La muhimu zaidi ya yote, wanachukulia wenyewe kama watu wateule, waliopewa kibali cha kufanikisha malengo yao kwa njia yoyote ile, ikiwa ni pamoja na hila na mauji ya halaiki. Zaidi ya hayo, kwa vile wanaamini katika wale mitume waporaji ambao *"....waliaangamiza nafsi zote kwa ncha ya upanga, hata walipokuwa wamewaangamiza wote, wala hawakumsaza mmoja mwenye kuvuta pumzi ..."*13

B. Wakristo

Inaweza kudhaniwa bila wasiwasi kwamba kuhusisha umbile la kibinadamu kwa Mwenyezi Mungu, kama inavyohubiriwa na Taurati, iliwavutia Wakristo kuamini kwamba Mungu ni kama baba ambaye alijitwalia mwana.

Huko Ulaya, ambako wengi wao wameukiri Ukristo na lile Agano la Kale likakubaliwa kama kitabu cha kwanza ndani ya Biblia, kuzaliwa na kuenezwa kwa tamaa ya anasa za dunia kunaweza kuhusishwa na dhana zisizo na mantiki kama hizo, ambazo zilishindwa kuwavutia wasomi.

C. Waislamu

Miongoni mwa Waislamu, kulikuwa na madhehebu mbili. Moja ilikuwa na mwelekeo kwa Ahlul-Bayt (A.S.), ambapo ile nyingine ilikuwa inapingana nao hao moja kwa moja. Hawa wa mwishoni wanaweza wakaitwa madhehebu ya watawala au Makhalifa. Madhehebu haya ya Makhalifa yaliamini katika kuwepo kimwili kwa Mwenyezi Mungu, kitu ambacho chenye kufanana na umbo la mwanadamu. Ni dhahiri, wazo hilo lilikuwa limeazimwa kutoka kwa Wayahudi, kama tutakavyothibitisha katika milango ifuatayo,

Inshallah.

Wakati dini ya kweli ya Mwenyezi Mungu inapochafuliwa kwa lugha yenye maneno ya kufuru, tunaziona dalili za athari za uharibifu katika zile imani halisi. Mafundisho ya Qur'ani Tukufu yalikuwa ya maneno machache ya dhahiri, halisi na wazi, lakini kwa vile wanazuoni wa Kiislamu walianza kuwakubali wale wasimulizi wa ngano wa Kiyahudi na Kikristo kama wafasiri wa Qur'ani Tukufu, hata zile itikadi kuu za Tawhiid zilishushwa na kuwa kama mambo ya kukisia tu.

Kabla hatujaendelea na mada yetu kuu, tunadhani kuna umuhimu wa kujadili yale matumiziya maneno halisi na ya kiistiari.

---

1. Tazama Tafsiir Ibn Kathiir, Juz. 4, uk. 17
2. Tabari (Toleo la Ulaya), Juz. 1, uk. 62–63.
3. Al–Gharaat, cha Thaqafi na vile vile Sharhe Nahjul Balaghah cha Ibn Abil Hadiid
4. Musnad ya Ahmad Hanbal
5. Tadhkiratul Huffadh cha Dhahabi
6. Tariikh Ibn Kathir, Juz. 8, uk. 109.
7. Usudul–Ghabah, Juz. 3, uk. 234 na Fat'hul–Bari, Juz. 1, uk. 166
8. Musnad Ahmad Hanbal, Juz. 2, uk. 195, 202. 203, na 209.
9. Wafayat al–A'yan
10. Tarikh Baghdad
11. Nukuu kutoka Kitabu cha Mwanzo; 3.
12. Nukuu kutoka Kitabu cha Mwanzo; 32.
13. Yoshua; 11: 14

Utangulizi (2): Maneno Halisi Na Yale Ya Kiistiari

Katika Kiarabu au Kifursi, kama vile katika lugha nyinginezo tu, pale neno linapoonyesha maana ambayo kwamba lilitungiwa kwa asili, matumizi yake yanaitwa halisi. Wakati tunaposema: "Mikono ya mwizi ilikatwa," neno "mikono" katika kadhia hii limetumika katika maana yake halisi.

Lakini pale neno linapotumika kama tamathali ya usemi ambamo linahamishiwa kwenye kitu ambacho halitumiki hasa, linaitwa la kitamathali au kiistiari. Kwa mfano, wakati neno "mkono" linapotumika kumaanisha "uwezo" au "mamlaka" na kadhalika.

Wakati mwingine inasemwa: *"Kuna mkono juu ya kila mkono."*

Katika suala hili, maana yake ni kwamba kuna uwezo juu ya kila uwezo. Matumizi kama hayo yanapatikana katika kila kazi ya fasihi, na inaongezea uzuri wa mtindo. Qur'ani Tukufu, katika mtindo

wake usioigika na bora sana, hutmia matumizi kama hayo katika sehemu nyingi.
Kwa mfano:

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا {29}

"Wala usifanye mkono wako* (*kama*) *uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjuwe mkunjuo wa kabisa ... (***Bani Israail; 17: 29***)

Lakini ni dhahiri kabisa kwamba maneno haya katika Ayah hii sio ya kutafsiriwa neno kwa neno. Maana ya Ayah hii ni: *"Usiwe bakhili, wala usiwe mkarimu mno au mbadhilifu...."*

Mfano mwingine ni wa neno *"Siraat"* ambalo katika Kiarabu lina maana ya "barabara" au "njia." Katika *Suratul–Fatiha*, kama tutachukua maana halisi ya neno *Siraat*, Ayah hiyo itasomeka hivi:

"Tuonyeshe barabara iliyonyooka. Barabara ya wale ulioshusha neema Zako juu yao, sio ya wale uliowaghadhibikia au waliopotea." (***Al–Fatiha***)

Kwa hakika, Ayah hizi hazizungumzii juu ya barabara zozote zile. Ayah zinazunguzia juu ya njia, ile njia ya Mitume, njia inayoongozea kwa Mwenyezi Mungu, ambayo ni sawasawa na Uislamu. Tunaomba tuonyeshwe njia ya wale waliobarikiwa na kuongozwa na sio ya wale ambao Yeye amewaghadhibikia.

Hitimisho

Kila mwanazuoni wa lugha ya Kiarabu atathibitisha kwamba ule "unyooshaji mkono mbele" katika Ayah ya Qur'ani Tukufu hakuelekezi kwenye viungo vya mwanadamu. Kunamaanisha utoaji mwingi wa tunzo au zawadi. Hali kadhalika, neno Siraat halirejelei kwenye zile barabara zenye mavumbi, linaelekeza kwenye njia ya kiroho na adhimu, Uislamu.

Hata wanazuoni wa wafasiri kutoka kwenye madhehebu tofauti na ile ya Ahlul–Bayt (a.s.) wanakubaliana nasi katika tafsiri hii. Hata hivyo, cha kushangaza zaidi, wakati neno linaloashiria sehemu za mwili kama vile "mkono", "jicho", au "kifundo cha mguu" linaonekana ndani ya Qur'ani Tukufu kuhusiana na Mwenyezi Mungu, wao wanasisitiza kwamba lazima lichukue maana halisi, na kwamba wao wanalitumia hasa kwenye viungo vya mwili "Wake." Madhehebu ya Ahlul–Bayt imeyachukulia maneno haya kuwa na maana ya kiistiari.

Kwa hiyo, ni muhimu kabisa kulinganisha na kupima hoja zinazotolewa na kila madhehebu, na kuchunguza ni vipi kila moja imepata kuungwa mkono na Qur'ani Tukufu na hadith. Hii itatuwezesha sisi kuzielewa zile Sifa Tukufu katika Uislamu.

Uchaguzi Wa Kitabu Kimoja Cha Tawhiid Kutoka Kila Madhehebu

Tumechagua kitabu kimoja kutoka kwenye madhehebu ya Makhalifa na kimoja kutoka madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.). Kila kimoja kinajishughulisha na maudhui ya Upweke wa Allah.

Tawhii kutoka kwa Ibn Khuzaimah ni ya kutoka madhehebu ya Makhalifa, na Tawhiid ya Sheikh Saduuq inawakilisha madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.). Kabla hatujaendelea na kunukuu kutoka kila kimoja chao, tunadhani ni busara tukiwatambulisha hao waandishi ili kwamba ubora na vyeo vyao viwe vinaeleweka.

Ibn Khuzaimah Kama Anayotazamwa Na Madhehebu Ya Makhalifa

Wanazuoni wamemteua Ibn Khuzaimah kama: Imamul Aimmah (Imam wa Maimamu)

● Al-Hafidh al-Kabiir (mtunzaji mkuu wa elimu za Kiislamu – au mashuhuri miongoni mwa wale walioihifadhi Qur'ani kwa moyo)

● Al-Mujtahid al-Mutlaq (Mwana-Fiqh thabiti)

● Bahrul Uluum (Bahari ya elimu)

● Ra'sul Muhaddithin (kiongozi wa wasimulizi)

● Habr ul-Ulama al-Amiliin (mshauri wa wanazuoni waadilifu)

● Ka'batul Ulama (kitovu cha wasomi)

Muhammad Ibn Ishaq Khuzaimah Nisaburi:

Yeye alizaliwa mnamo mwaka wa 213 Hijiria na alifariki mwaka wa 311 Hijiria. Wanazuoni wengi wamesimulia hadithi kutoka kwake, ikiwa ni pamoja na waandishi wa Bukhari na Muslim. Inasemekana kwamba Ibn Khuzaimah kwa kulipa hisani alizikubali hadithi zilizosimuliwa na hawa wawili wa mwisho hapo juu.

Mbali na tasnifu ndogo ndogo zilizoandikwa katika kujibu maswali fulani, Ibn Khuzaimah ameandika vitabu vikubwa 140, ambavyo vinajumuisha pamoja na ile *Sahih* maarufu ya Ibn Khuzaimah. Baadhi ya Wanazuoni wanaiona Sahih yake kama ni bora na yenye kuzidi aula kuliko *Sahih Bukhari* na *Sahih Muslim*. Alikuwa ni mfuasi wa Shafi'i.

Ndani ya mjala huu mfupi, tumetegemea kwenye kitabu chake kiitwacho *Tawhiid*, kilichopitiwa kwa makini na Muhammad Khaliil Haras wa al- Azhar, Cairo na kuchapishwa na *al-Azhar University Press* – (Taasisi ya kupiga chapa ya Chuo Kikuu cha al-Azhar), Cairo, mnamo mwaka 1378 Hijiria.

Sheikh Saduuq Kama Anavyotazamwa Na Madhehebu Ya Ahlul-Bayt (A.S.)

Saduuq ni jina alilopewa Abu Ja'far Muhammad ibn Ali bin Husayn bin Babawayh Qummi. Yeye alifariki mnamo mwaka 381 Hijiria. Ni mwanazuoni mwenye heshima ya juu, asiyehitaji kutambulishwa. Ameandika takriban vitabu 200.

Katika mjadala huu, tumetegemea kwenye kitabu chake cha *Tawhiid*, kilichochapishwa Tehran mnamo mwaka 1381 Hijiria, kikapitiwa kwa tahaki- ki na Syed Hashim Husayni Tehrani.

Vitabu hivi viwili ndio vyanzo vyetu vikuu. Kwa nyongeza, tunarejea kwenye vitabu vingine maarufu vilevile kama vile Mlango wa Tawhiid ndani ya *Sahih Bukhari*, Mlango wa ***Iman*** kutoka Sahih Muslim. Na kwa upande wa madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.), tutafanya marejeo kwenye Mlango wa Tawhiid kutoka kitabu Biharul Anwar cha Majlisi (aliyefariki mwaka 1111 Hijiria).

Sura Ya Kwanza: "Mfano" Wa Mwenyezi Mungu

(A) Kutoka Madhehebu Ya Makhalifa

Hebu tuzichunguze hadithi mbili kutoka kwenye madhehebu hii:

1. Ibn Khuzaimah ndani ya Tawhiid, pamoja na Bukhari na Muslim wanasimulia kupitia kwa Abu Huraira kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema:

"Allah amemuumba Adam kwa mfano Wake Mwenyewe, futi sitini kwa urefu. Halafu Akamuamuru yeye kwenda mbele ya kikundi cha Malaika na kuwasalimia. 'Wasikilize vizuri wakati wanapojibu maamkuzi yako, kwani hayo yatakuwa ndio maakuzi wewe na kizazi chako mtakayotu- mia,' Allaha akasema.

"Hivyo Adamu akatii na akawaamkia hivi: 'Assalamu Alaikum' (Amani iwe juu yenu). Hao Malaika wakamjibu: 'Assalamu Alaika wa Rahmatullah.' (Amani iwe juu yako na Rehma za Mwenyezi Mungu), wakiongezea 'Wa Rahmatullah.'

"Hivyo kila mmoja anayeingia peponi atakuwa katika mfano wa umbile la Adam. Wanadamu walipunguzwa tarat- ibu katika urefu kiasi muda ulivyopita, hadi kufikia kimo walichonacho leo hii."

2. Abu Huraira anasimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema:

"Wakati wowote ule mtu anapohusika kwenye ugomvi au mapigano dhidi ndugu yake, mtu anapaswa kujiepusha kumpiga kwenye uso. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu alimuumba Adam katika mfano Wake Mwenyewe."1

Hizi ni hadith kutoka kwa Abu Huraira. Hebu sasa tuzilinganishe na hadithi zilizosimuliwa na Madhehebu ya Ahlul–Bayt (a.s.) ili picha ipate kukamilika.

(B) Ahlul–Bayt (A.S.) Wanauelezea Ukweli Hasa

1. Husayn bin Khalid anasema:

"Nilimuuliza Imam Ridha (a.s.) kuhusu ile hadithi mashuhuri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba Mwenyezi Mungu alimuumba Adam katika mfano Wake Mwenyewe. Yeye akasema: 'Walaaniwe wale wasimuliaji wadanganyifu ambao wameiacha ile sehhemu ya kwanza ya hadithi hii.' Kisha akaelezea: Wakati mmoja Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anapita pale aliposikia watu wawili wakitukanana wenyewe kwa wenyewe. Alimsikia mmoja wao akisema kwamba: 'Mwenyezi Mungu auchukize na kuufedhehesha uso wako, na uso ambao unafanana na wako.'

Wakati huo, Mtukufu Mtume akasimama na kuwaonya kwa kusema: 'Usitamke maneno kama hayo kumwambia ndugu yako. Kwani Mwenyezi Mungu amemuumba Adamu (pia) kwa mfano wake. (Akimaanisha kwamba Adamu vilevile alifanana na huyo ndugu yake)."

2. Katika hadithi nyingine iliyosimuliwa na Abul Ward kwa Thamamah kutoka kwa Amirul Mu'minin Ali ibn Abi Talib (a.s.) tunasoma kama ifuatavyo:

"Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimsikia mtu mmoja anamtukana mwingine akisema kwamba: 'Mwenyezi Mungu auchukize na kuufedhehesha uso wako, na uso unaofanana na wako.' Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: 'Nyamaza kimya! Usisema maneno kama hayo! Kwani Mwenyezi Mungu alimuumba Adamu katika mfano wake.'"

3. Licha ya hadithi hizi mbili, hebu natuchunguze nyingine moja zaidi, ambayo itatupa maoni ya jumla juu ya jinsi Maimamu wa Ahlul–Bayt (a.s.) walivyoziangalia imani za uhusishaji viungo kwa Allah (*anthropomorphism*).

Saduuq katika kitabu chake cha *Tawhiid* anasema:

"Imam Musa ibn Ja'far (a.s.) alipokea barua ambayo ndani yake mtu mmoja alikuwa akitafuta ubainisho kuhusu ile imani inayohusu mwili na mfano wa Mwenyezi Mungu. Imam (a.s.) akamjibu: 'Sifa zote zimwendee Allah swt! Hakuna chochote kile kinachofanana na Yeye – hakuna mwili na wala hakuna mfano.'"

(C) Uchunguzi Na Ulinganishaji

Tunapotafakari juu ya hadithi hizi na kuzilinganisha, tunakuta kwamba Abu Huraira katika hadithi zake mbili ameweka nyongeza mbili na ameacha jambo moja.

1. Lile Ambalo Limeachwa

Wakati Abu Huraira anaposimulia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), yeye analiacha lile tukio ambamo Mtume alikabiliana na watu wawili waliohusika katika lugha chafu na matusi, halafu akamuonya mmoja wao asiizungumzie vibaya sura ya mwanadamu kwa sababu ilifanana na ile ya Adam. Kwa hakika jambo lililoachwa hapa ni muhimu sana, kwa sababu maelezo ya Abu Huraira yanatoa taswira kwamba kile kiwakilishi nomino "yake" kinarejea kwa Mwenyezi Mungu, ambapo kwa kweli kinarejea kwa yule mtu mwenyewe.

Abu Huraira anaweza kuwa ameacha ile sehemu muhimu ya hadithi hiyo kwa sababu:-

(**a**) Alikuwa akihifadhi hadithi kichwani, kwa vile alivyokuwa hawezi kusoma wala kuandika. Na hata kama angekuwa anaweza, asingeruhusiwa na hao Makhalifa ambao walikuwa wamewakataza Waislamu kutunza kumbukumbu ya maandishi ya hadithi za Mtume, hadi mwisho wa karne ya kwanza ya Hijiria.

(**b**) Abu Huraira alikuwa ameshawishiwa sana na Ka'b al-Ahbar ambaye alieneza hadithi fupi zilizopotoshwa kutoka kwenye Taurati miongoni mwa Waislamu. Ni dhahiri, athari za kile alichokisimulia Ka'b zilikuwa bado zina nguvu mpya kwenye akili ya Abu Huraira, kwa sababu kimekuja takriban miaka ishirini baada ya kukisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

(**c**) Huenda kosa lilikuwa upande wa wasimulizi wa siku za baadae ambao walizinakili simulizi za Ka'b zilizohusishwa kwa makosa kwa Abu Huraira. Vyovyote vile hali iwavyo, matokeo yake yanabakia vile vile, bila kubadilika.

2. Nyongeza Mbili

(**a**) Katika hadithi ya kwanza, Abu Huraira anayahusisha maelezo yafu- atayo kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):-

"Wakati wowote mtu anaposhiriki katika ugomvi dhidi ya ndugu yake, huyo ajiepushe na kumpiga usoni mwake....."

Inawezekana hii ni hadithi mbadala iliyobuniwa na Abu Huraira, mahala pa ule uachwaji tulioutaja hapo juu.

(**b**) Katika hadithi nyingine, Abu Huraira anazungumzia juu ya urefu wa Adam:-

"Mwenyezi Mungu amemuumba Adam katika mfano Wake,
kwa urefu wa futi sitini....."

Ni dhahiri, maelezo kama haya si yenye ukweli, wala hayapatani na uchunguzi wa kielimu.

Mtu anaweza kuona kwa urahisi kwamba hadithi zilizosimuliwa kutoka kwa Abu Huraira zinabeba kufanana kunakoafikiana sana na zile hadithi kutoka kitabu cha Mwanzo ndani ya Agano la Kale.

Kwa kuzichezea zile hadithi za kweli za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kuingiza maneno hapa na pale, kukata hapa na pale, Abu Huraira na wanaofanana naye wamefanikiwa kutoa usadikikaji kwenye hadithi za uzushi kutoka kwenye Taurati. Hizi, hivyo basi, ndio hadithi Israiliyyat, ambazo zimefanya uingiliaji wa kuhuzunisha kwenye hadithi na imani za Kiislamu.

Madhehebu za Makhalifa zimezimeza, kuanzia ndoano, kamba yake na chambo chake, kwa sababu majina maarufu kama yale ya akina Abu Huraira yameambatanishwa nazo.

Matokeo yake yamekuwa kwamba mahali popote pale maneno kama “uso” yanapotokea kuhusiana na Mwenyezi Mungu ndani ya Qur’ani Tukufu, wao wamesisitiza juu ya maana halisi. Kwao wao, sifa zote za kibinadamu, kanuni na maumbo vinaweza kutumika kwa Mwenyezi Mungu! Tutalijadili somo hili katika milango inayofuata Inshallah.

---

1. Sahih Muslim, uk. 2016, 2017

Sura Ya Pili: “Uso” Wa Mwenyezi Mungu

1. “Uso” Wa Mwenyezi Mungu Kama Unavyoeleweka Kwa Madhehebu Ya Makhalifa:

Ibn Khuzaimah katika kitabu chake kiitwacho Tawhiid anaandika katika ukurasa wake wa kumi. Mlango unaothibitisha uso wa Mwenyezi Mungu, ambao Yeye Mwenyewe ameueleza kama wenye kujaa utukufu na heshima katika Ayah ifuatayo:

وَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ {27}

“Na itabaki dhati ya Mola Wako, Mwenye utukufu na Heshima.” (***Ar- Rahmaan; 55: 27***)

Na Amethibitisha vilevile kwamba Uso Wake hautatoweka kamwe:

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ ۚ لَهُ الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ {88}

"..... Kila kitu kitaangamia isipokuwa Uso Wake, hukumu iko Kwake, na kwake Yeye mtarejeshwa." **(*Al-Qasas; 28: 88*)**

Baada ya hapo, Ibn Khuzaimah anatafuta uhakikisho mwingine zaidi kuto- ka kwenye Ayah nyingine za Qur'ani Tukufu, na kisha anasema:

"Kwa hiyo Mwenyezi Mungu amethibitisha kabisa kwamba Yeye anao uso, ameuelezea kama ni Wenye Utukufu na Heshima, na amehukumu kwamba uso huo utadumu milele, bila kutoweka kamwe....."

Katika maelezo yake ya kumalizia, anaongezea kusema:

"Kila kile ambacho Mwenyezi Mungu amejithibitishia yeye Mwenyewe, sisi pia tunakithibitisha. Lakini uso Wake sio kama uso wowote wa kiumbe chochote."

Katika ukurasa wa kumi na moja wa kitabu hicho hicho, Ibn Khuzaimah anasimulia hadithi 14 kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambamo neno "uso" limetajwa, na anaegemeza madai yake juu ya hadithi hizo. Kwa mfano, pale Mtume anapoomba du'a kwa kusema:

"Ninaomba hifadhi kwa Uso Wako wenye Rehma."

Ibn Khuzaimah anaona kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alilitaja neno uso kwa maana yake halisi. Kwa maneno mengine, anasisitiza kwamba "uso" ni sehemu ya mwili wa Mwenyezi Mungu, sawa sawa na ule wa mwanadamu au mnyama mwingine.

Sasa hebu tuangalie kile ambacho Ahlul-Bayt (a.s.) walichokieleza katika hadithi zao:

2. "Uso" – Kama Ulivyoelezewa Na Ahlul-Bayt (A.S.)

Kama dibaji, hebu natushughulike na hadithi kutoka kwa Amirul- Mu'minin, Ali bin Abi Talib (a.s.) ambamo aliweka kanuni kwa ajili ya uelewa wa Ayah za Qur'ani Tukufu, hususan zile zinazohusika na sifa za ki-mungu.

Mtu mmoja alipeleka swali lake kwa Ali bin Abi Talib (a.s.), akinukuu baadhi ya Ayah kutoka kwenye Qur'ani Tukufu, kutoa vipingamizi vyake. Miongoni mwa hizo tunachagua hizi mbili zifuatazo:

Maana hasa ya maneno yenyewe ya Ayah hizi mbili ni:

وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا {22}

*“(**Na katika hiyo Siku ya Kiyama**) **Na akaja Mola Wako na Malaika safu kwa safu …”*
(***Al-Fajr; 89: 22***)

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِيَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ {158}

“Hawangoji ila wawafikie Malaika au Mola Wako afike, au zifike baadhi ya dalili za Mola Wako ……” (***Al-An’aam; 6: 158***)

Swali lililoletwa ni kama Mwenyezi Mungu Mwenyewe atakuja kutokeza hiyo Siku ya Kiyama, kwa dhahiri kama ilivyowasilishwa na Ayah hizo.
Imam Ali (a.s.) alielezea hivi:

“Chochote kile ambacho Mwenyezi Mungu, Aliye Mkuu, amekidhihirisha ndani ya Ayah, ni kweli kabisa; isipokuwa kwamba kuja kwake sio sawa na kuja kwa viumbe Vyake. Nimekushauri hapo mapema kwamba sehemu fulani za Qur’ani Tukufu lazima zisitafsiriwe kwa maana halisi ya maneno; badala yake unapaswa kuelewa ile maana ya ki- istiari. Neno Allah sio kama neno la kibinadamu, na tendo Lake sio kama tendo la kibinadamu. Ili kuiweka hoja yangu ieleweke vizuri, nitakupa mifano kutoka kwenye Qur’ani Tukufu, ili Inshallah, uelewaji wako wa Qur’ani utakuwa wa hakika na wa sawasawa. Qur’ani inamsimulia Nabii Ibrahim akisema:

وَقَالَ إِنِّي ذَاهِبٌ إِلَىٰ رَبِّي سَيَهْدِينِ {99}

“Nakwenda kwa Mola Wangu, yeye ndiye atakayeniongoza.” (***As- Saffat; 37: 99***)

Hapa, “kwenda kwa Mola” hakuna maana ya kutembea hadi Kwake kwa msaada wa miguu. Ina maana ya kurejea Kwake, kwa uimara na ukweli, kupitia ibada, na kutafuta ukaribu Naye. Je, unaweza kuona tofauti baina ya maana yake halisi na ile maana yenyewe iliyowasilishwa na istiari? Halafu tena, maana halisi ya Ayah zifuatazo inaweza kuwa:

وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ الْأَنْعَامِ ثَمَانِيَةَ أَزْوَاجٍ ۚ {6}

“…na akakushushieni wanyama, (kwa jozi) wanane madume na majike …” (***Az-Zumar; 39: 6***)

وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ {25}

"....Na tumekishusha chuma chenye nguvu nyingi ..." **(*Al-Hadiid; 57: 25*)**

Sasa kama ungekuwa utegemee kwenye maana halisi, ungeona kwamba zile jozi nane za ng'ombe na kile chuma "vilishushwa" kutoka juu mbinguni. Lakini bila shaka haikumaanishwa hivyo. Maneno hayo hapa yanamaanisha "tuliumba," au "Aliumba."1

Ali ibn Abi Talib (a.s.) ametufundisha kanuni mbili muhimu juu ya kuele- wa Sifa na kazi za Mungu. Kwanza, kazi na matendo ya Mwenyezi Mungu haviwezi kulinganishwa na kazi na matendo yetu. Wakati Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani Tukufu anaposema:

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ {1}

"Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia..." **(*Al-Mujadilah; 58:1*),**

Haifananishwa na kusikia kwa mwanadamu, mnyama au kiumbe chochote. Sisi tunasikia kwa msaada wa masikio yetu. Kusikia kwa Mwenyezi Mungu hakuashirii kitu kama hicho.

Mwenyezi Mungu anasema:

قَالَ يَا إِبْلِيسُ مَا مَنَعَكَ أَنْ تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ {75}

"Akasema: Ewe Iblis, ni nini kimekuzuia kumtii yule niliyemuumba kwa mikono yangu?
(*As-Swad; 38: 75*)

Mwanadamu anaweza akasema vile vile kwamba ameumba kitu kwa mikono yake. Lakini yote yana maana tofauti. Mwenyezi Mungu hana viungo, wala hahitaji mikono.

Mwenyezi Mungu alimdhihirishia Nabii Musa (a.s.) hivi:

قَالَ لَا تَخَافَا ۖ إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَىٰ {46}

"Msiogope, bila shaka mimi niko pamoja nanyi, ninasikia na ninaona." **(*At-Twaha; 20: 46*)**

Kuwa pamoja na mtu kuna maana tofauti wakati inapotumika kwetu sisi. Wakati Mwenyezi Mungu yuko "pamoja" na mtu, haiashirii kuwa pamoja kimwili au kwa ukaribu.

Pili, Amirul Mu'minin, Ali bin Abu Talib (a.s.) alisema kwamba ilikuwa ni lazima kuyaelewa matumizi

halisi na yale ya kiistiari vilevile ya maneno ndani ya Qur'ani Tukufu, kabla mtu hajaanza kutafsiri au kusherehesha. Alitoa mifano miwili kutoka ndani ya Qur'ani ili kuielezea hoja yake.

Kwa kweli, tunapokaa kusoma kazi ya sanaa ya fasihi au maandishi, katika lugha yoyote ile iwayo, tunatakiwa kuwa wenye kufahamu vizuri zile tamathali za semi, matumizi tofauti ya maneno na kadhalika. Kwa kutegemea kanuni hii iliyoenea pote, hebu sasa tuangalie jinsi madhehebu ya Ahlul–Bayt (a.s.) inavyoushughulikia huu mtajo **"uso"** wa Mwenyezi Mungu.

Abu Hamza alimuuliza Imam Muhammad Baqir (a.s.) kuhusu maana ya Ayah hii:–

"Kila kitu chenye uhai kitatoweka isipokuwa Uso Wake Mwenyewe."

Imam alimjibu hivi:

"Hivi wao wanadhania kwamba Mwenyezi Mungu anao uso na kwamba kila mtu atakufa na kutoweka bali Uso Wake? Mwenyezi Mungu yuko mbali na kuwa mwenye uso! Maana halisi ya Ayah hii ni kwamba kila kitu kitatoweka isipokuwa dini ya Mwenyezi Mungu, mwelekeo na njia, ambayo inaongozea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Katika hadithi nyingine kutoka kwa Imam Ja'far as–Sadiq (a.s.), Ayah hii imeelezewa zaidi:

"Kila kitu kitatoweka isipokuwa kule kutwaa njia iliyonyooka."

Maelezo yote yanaelekeza kwenye jambo moja lile lile, njia iliyonyooka au dini ya Mwenyezi Mungu. Hivi ndiyo jinsi Madhehebu ya Ahlul–Bayt (a.s.) inavyokitafsiri hiki kifungucha maneno "uso wa Mwenyezi Mungu."

1. *Wajh* likimaanisha "ule mwanzo" au "sehemu ya mwanzoni" kama ilivyotumika katika *Wajhun Nahar* – yaani asubuhi.

2. *Wajh* likimaanisha "ukweli au dhati ya jambo" – kama wanavyosema katika Kiarabu, *Asaba Wajhal Masa'lah* – yaani Alikuja kwenye sehemu ya jambo ambayo ni ngumu kutatulika.

3. *Wajh* likimaanisha "mwelekeo, lengo," kama: *Ittajahat Tijaraj* – yaani alilenga kufanya biashara.

Wanazuoni wa Kiarabu wa kisasa wamethibitisha maana hizi vilevile, kama wale waandishi wa Mu'jamu Alfaadhil Qur'an al–Karim, kilichochapishwa kutoka Misri mnamo mwaka 1390 A.H.

Kwa kuzingatia zile maana mbali mbali zilizoambatanishwa na neno Wajh madhehebu ya Makhalifa haikuwa na sababu yenye kueleweka kugandamana kwenye maana moja, ambayo iliyopendekeza kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa na viungo vya kimwili, kwa namna ile ile kama sisi wanadamu tulivyonavyo.

Ni wazi kabisa kwamba waliathiriwa na ule utomaji maneno yasiyokuwemo wa Kiyahudi na kwa hadithi

kama hizo, ambazo zilihusishwa kwa masahaba kama vile Abu Huraira.

Katika mjadala huu mfupi, tunatambua kwamba madhehebu mbili zina maoni yanayoachana kabisa kuhusu Mwenyezi Mungu. Moja inaamini katika uhusishaji viungo kwa Mwenyezi Mungu (*anthropormophism*) ikimdhania Yeye kwamba ni kama sisi, au kama kiumbe kingine chochote kile, akiwa na viungo na kano. Na hii nyingine inaamini Nafsi ya juu sana na tukufu, isiyolinganishika kwa hali yoyote ile na maumbile.
Kuna Ayah ndani ya Qur'ani Tukufu, ambazo zinahitaji msaada wa kimungu kuweza kuzielewa, na kwamba msaada huo unakuja kupitia kwa Mtume (s.a.w.w.) au kwa Ahlul-Bayt wake halisi na watoharifu kabisa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخَرُ مُتَشَابِهَاتٌ ۖ فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ ابْتِغَاءَ الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاءَ تَأْوِيلِهِ ۗ وَمَا يَعْلَمُ تَأْوِيلَهُ إِلَّا اللَّهُ ۗ {7}

"...ndani yake zimo Ayah zilizo wazi wazi nazo ndizo msingi wa Kitabu, na nyingine ni zenye kufichikana. Basi wale ambao katika nyoyo zao mna upotovu, hufuata zile zilizofichikana katika hayo kwa ajili ya kutaka upotovu na kutaka kutafsiri watakavyo. Na hakuna ajuaye tafsiri yake ila Mwenyezi Mungu ..." (***Aali Imran; 3: 7***)

Mwenyezi Mungu amemkabidhi Mtume Wake (s.a.w.w.) wajibu wa kuielezea maana yote ya Qur'ani Tukufu:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ {44}

"...Tumekuteremshia Qur'ani ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwa ajili yao ..."
(***An-Nahl; 16: 44***)

Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameigawa elimu yake kwa Ali bin Abi Talib (a.s.) ambaye ameinakili na akaihifadhi kwa moyo kwa uaminifu kabisa. Baada ya kufariki kwa Mtukufu Mtume wetu (s.a.w.w.), Waislamu walirejea kwa Ali (a.s.) kila ambapo tatizo au ugumu ulijitokeza kuhusiana na kuielewa Qur'ani Tukufu; na wakati wote alitoa majibu ya kutosheleza. Elimu ambayo waliyonayo Ahlul-Bayt (a.s.) ni ya kimungu. Haitegemei kwa hali yoyote ile juu ya maoni ya mtu au tafsiri za wanazuoni ambao badala yake waliathiriwa na dhana zisizo za Kiislamu.

Mlango unaofuata utaweka tofauti hizi kwenye muonekano dhahiri hasa.

1. Kitabu Tawhiid cha Saduuq, uk. 265

Sehemu Ya Tatu: Macho Ya Mwenyezi Mungu

1. “Macho” Ya Mwenyezi Mungu Kama Yanavyoeleweka Kwa Madhehebu Ya Makhalifa

Katika vitabu vya *Tafsir* na hadith, wanazuoni wa madhehebu hiyo hapo juu wamesimulia kutoka kwa Abu Huraira ambaye amesema, wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipozisoma Ayah zifuatazo:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ ۚ إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُمْ بِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا {58}

“Hakika Mwenyezi Mungu anawaamuruni kurejesha amana kwa wenyewe, na mtakapohukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.” **(*An- Nisaa; 4: 58*)**

“Niliona kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akionyesha wazi kusikia na kuona kwa Mwenyezi Mungu kwa kuweka dole gumba lake juu ya masikio yake na kidole chake cha shahada juu ya jicho lake.”

Wakati Abu Huraira aliposimulia hadithi hiyo hapo juu, aliurudia ule udhihirishaji kwa kuweka vidole vyake mwenyewe juu ya sikio na jicho lake. Alifanya hivyo kusisitiza kwamba Mwenyezi Mungu anasikia kwa msaa- da wa masikio na anaona kwa kusaidiwa na macho yake.

Jahmiyyah ilikuwa ni madhehebu, ambayo ilizishutumu na kuzikataa dhana kama hizi. Katika ukanushaji kwa madhehebu ya *Jahmiyyah,* Abu Dawuud anaandika katika *Sunan* yake maarufu kama ifuatavyo:

“Hadithi hii ya Abu Huraira inazikanusha imani za *Jahmiyyah* (ambao wanaamini kwamba Mwenyezi Mungu hana viungo, wala hana mwili)”
Ubunifu wa maneno ya uwongo wa Abu Huraira umeipelekea madhehebu ya Makhalifa katika kuamini kwamba popote pale hili neno ***Ayn*** linapotokeza kwenye Qur’ani Tukufu kuhusiana na Mwenyezi Mungu, ni lazima lieleweke kama jicho lenyewe hasa – sehemu ya mwili ambayo hutazama na kuona. Kwa hiyo tunakuta Ibn Khuzaimah, Imam wa Maimamu kama anavyotukuzwa na madhehebu yao, akisimamisha mlango wa pekee katika kitabu chake cha Tawhiid, kuthibitisha kwamba Mwenyezi Mungu, Aliye juu

kabisa, anayo macho. Yeye anaandika hivi:

“Tunarudia kusema kile Mwenyezi Mungu Mwenyewe alichokisema kwenye Kitabu Chake na kile Mtume Wake (s.a.w.w.) wa kuheshimika alichokithibitisha juu ya Mwenyezi Mungu kuwa na macho.”

Baada ya hapo, anaendelea kunukuu Ayah zifuatazo:

i) Mwenyezi Mungu alimwambia Nabii Nuh (a.s.):

وَاصْنَعِ الْفُلْكَ بِأَعْيُنِنَا {37}

“Na tengeneza jahazi mbele ya macho Yetu ... **(*Huud; 11:37*)**

ii) Akizungumzia Jahazi la Nabii Nuh:

تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا {14}

“Ikaenda mbele ya macho Yetu ... **(*Al-Qamar; 54: 14*)**

iii) Aliyoyazungumza kwa Nabii Musa (a.s.):

وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِنِّي وَلِتُصْنَعَ عَلَىٰ عَيْنِي {39}

“Na nimekirimu mapenzi yangu juu yako ili upate kulelewa machoni Mwangu.”
(*At-Twaha; 20: 39*)

iv) Aliyoyazungumza na Mtume wetu (s.a.w.w.)

وَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا {48}

“Na ingoje hukumu ya Mola Wako, hakika wewe uko mbele ya macho yetu ...” **(*At-Tuur; 52: 48*)**

Ibn Khuzaimah anasema:

“Kwa kuzingatia Ayah hizi kutoka ndani ya Qur’ani Tukufu, ni wajibu juu ya kila Mu’min kuthibitisha imani

ya kwamba Mwenyezi Mungu anayo macho, na hayo ameyathibitisha Yeye Mwenyewe. Na yoyote yule ambaye haamini yale Mwenyezi Mungu aliyoyadhihirisha ndani ya Kitabu Chake, na kile alichojihusisha Kwake Mwenyewe, kwa kweli huyo sio Mwislamu. Maana Qur'ani imedhihirishwa vya kutosha na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe, kwani Mwenyezi Mungu amemuamrisha yeye ndani ya Qur'ani Tukufu hivi:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ {44}

"...Tumekuteremshia Qur'ani ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwa ajili yao ..."
(***An-Nahl; 16: 44***)

"Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika tafsiri yake ameeleza wazi wazi kwamba Mwenyezi Mungu anayo macho maw- ili! Tafsiri yake inakubaliana na maneno ya Qur'ani Tukufu,

Qur'ani hii hii ambayo iko katika muundo wa kitabu baina ya majalada mawili, na inasomwa ndani ya Misikiti na vyuo."

Akiwa hakutosheka na hoja hiyo, anakimbilia kwenye hadithi, miongoni mwazo ni ile moja kutoka kwa Abu Huraira. Mwishowe, anatoa simulizi ifuatayo kutoka kwa Abdullah ibn Umar:

"Mtume (s.a.w.w.) amesema: Mwenyezi Mungu sio kipofu katika jicho moja, kama Dajjal ambaye jicho lake la kulia halioni. Linaning'inia kama mbegu ya zabibu."

2. Hilo "Jicho" Kama Lilivyoelezwa Na Ahlul-Bayt (A.S.)

Maimamu wa Ahlul-Bayt (a.s.) wametoa maana halisi ya Ayah hizi. Hata hivyo, ni lazima tushughulike na somo hili kwa maelezo kiasi juu ya mistari ile.

Ibn Khuzaimah amelichukulia neno *Ayn* au *A'yunina* kwa maana halisi, kuthibitisha madai yake kwamba yanaashiria macho ya Mwenyezi Mungu. Ukweli ni kwamba neno *Ayn* na yatokanayo nalo yana maana kadhaa katika lugha ya Kiarabu. Kwa maelezo zaidi mtu anaweza kurejea kwenye kamusi maarufu, *Lisanul Arab*. Katika *Mu'jamul Udaba* Juz. 2, uk. 11, tunakuta taabini (maneno ya kusifu) ya Ibn Faris Ahmad bin Zakariyya (aliyefariki mwaka wa 369 Hijiria) ambamo ndani yake kila ubeti unaishia na neno *Ayn*, kila moja likiwa na maana tofauti. Syed Muhsin al-Amiin anayo taabini kama hiyo yenye beti sitini.

Qur'ani Tukufu imelitumia neno hilo katika maana zote mbili, maana halisi na ile ya kiistiari vile vile. Katika sehemu ishirini na moja, Qur'ani Tukufu inalitumia neno *Ayn* kumaanisha kijito cha maji au mto.

Lakini jambo la muhimu ni kwamba zile Ayah zilizonukuliwa na Ibn Khuzaimah kuhakikisha imani yake zote zina maneno hayo yakitumika katika maana ya kitamathali.

Kwa Kiingereza tunasema: *To keep an eye on* (angalia kwa makini), ikiwa na maana ya kufanya uangalizi kwa makini; *in the eyes of the law,* (kufuatana na sheria), ikiwa na maana kwa maoni au uamuzi wa kisheria; *the eye of the dome* (kwa jicho la kuba), ikimaanisha katika sehemu yake kuu – na kadhalika. Ni dhahiri, matumizi kama haya sio ya maana halisi. Vivyo hivyo, maneno haya yametumika kuashiria maana zao za kiistiari.

Katika kitabu maarufu, Majma al–Lughat al–Arabiyyah kilichochapishwa Misri, tunakuta haya:

"Ndani ya Qur'ani Tukufu, neno Ayn limetumika katika maana halisi na ile ya kiistiari vile vile. Kwa mfano, katika Ayah:

وَقَالَتِ امْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرَّتُ عَيْنٍ لِي وَلَكَ ۖ {9}

***i*) *"Na mkewe Firaun akasema: Ni kiburudisho cha macho kwangu na kwako ...*(*Al–Qasas; 28: 9*)**

فَكُلِي وَاشْرَبِي وَقَرِّي عَيْنًا ۖ {26}

***ii*) "(*Kwa Maryam*) *Basi ule na unywe na uburudishe macho yako...*(*Maryam; 19: 26*)**

Ni dhahiri kwamba hapa vifungu vya maneno vilivyotumika na *Aynan* na *Aynin* vyote vinawakilisha furaha na kuridhika.

Historia inatuambia kwamba Mwenyezi Mungu alimuamuru mama yake Nabii Musa (a.s.) kumtupa ndani ya mto. Musa (a.s.) kama mtoto mchanga alilifikia kasiri la Firaun juu ya mawimbi ya mto huo, ili kulelewa naye kama mwana. Maelezo kamili ya Ayah hiyo ni:

وَقَالَتِ امْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرَّتُ عَيْنٍ لِي وَلَكَ ۖ لَا تَقْتُلُوهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ {9}

***"Na mkewe Firaun akasema: Ni kiburudisho cha macho kwangu na kwako, msimuue, huenda atatunufaisha, au tumpange kuwa mtoto hali hawatambui."* (*Al–Qasas; 28: 9*)**

Katika mfano wa pili, Ayah inazungumza na Maryam, mama yake Nabii Isa (a.s.). pale alipomzaa Isa (a.s.) alihuzunika kwa sababu alijua kwamba watu hawatamuamini kwamba alikuwa bikira, na kwamba Isa (a.s.) alizaliwa bila baba, kwa amri tukufu ya Mungu. Hivyo Mwenyezi Mungu anasema:

“Usihuzunike! Kwani Mola wako amekupatia kijito cha maji chini yako – na litikise shina la mtende, litakushushia tende zilizoiva. Basi ule na unywe na uburudishe macho yako.”

Sasa zile Ayah zilizonukuliwa na Ibn Khuzaimah nazo zinahitaji uchambuzi kidogo vile vile. Ayah ya kwanza, ilizungumzwa kwa Nabii Nuh (a.s.). Maana yake sahihi ni:

“Tengeneza Jahazi chini ya uangalizi na ulinzi wetu.”

Ayah ya pili vile vile ina maana kwamba Jahazi la Nuh linaelea chini ya uangalizi na ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Na katika Ayah ya tatu, Mwenyezi Mungu anadhihirisha kwa Musa (a.s.), maana sahihi ya Ayah ni:

“Na niliyakirimu mapenzi yanggu juu yako ili kwamba uwe unalelewa chini ya ulinzi na uangalizi Wangu.....”

Hatimae, ile Ayah ya nne iliyozungumziwa kwa Mtukufu Mtume wetu (s.a.w.w.) ina maana kwamba:

“(Ewe Mtume!) – Na ingoje hukumu ya Mola Wako kwa subira, kwani wewe ni kipenzi Chetu na hivyo umelindwa.”

Mwisho kabisa ile hoja kwamba Mwenyezi Mungu sio kipofu kama Dajjal (mpinga Kristo). Vema, hii inatudokezea sisi kwamba yeye anatutaka sisi tuamini kwamba Mwenyezi Mungu anayo macho Yake, mwenye afya na asiyedhurika! Kwa kuzingatia mazungumzo yetu ya hapo juu, tunaweza kudhania ni jinsi gani hadithi hii ingeweza kusadikika! Tumekwisha kuonyesha tayari ni jinsi gani Abu Huraira asivyoaminika na jinsi askari wake walivyokuwa, na walivyokuwa chini ya athari za uenezaji wa Kiyahudi na Kikristo.

Ile itikadi halisi ya Kiislamu kwa hiyo ilivurugwa na hadithi potofu zilizokuwa na msingi juu ya Taurati iliyotomwa maneno yasiyokuwemo na maandishi mengine yasiyokuwa ya Kiislamu

Sura Ya Nne: “Mikono” Ya Mwenyezi Mungu

“Mikono” Ya Mwenyezi Mungu Kama Ilivyosimuliwa Na Madhehebu Ya Makhalifa.

Wanazuoni wa madhehebu hiyo hapo juu wamesimulia ndani ya vitabu vyao kutoka kwa Abu Huraira ambaye amesimulia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama ifuatavyo:

“Adamu na Musa walikuwa na mazungumzo yafuatayo: Musa alisema: ‘Ewe Adamu! Mwenyezi Mungu

alikuumba kwa mikono Yake Mwenyewe… Lakini uliwateremsha wanadamu kutoka kwenye bustani kwa sababu ya dhambi yako.'

Adamu akajibu: 'Ewe Musa, Mwenyezi Mungu kwa hakika amekutukuza wewe, na akaandika Taurati kwa ajili yako kwa mikono Yake Mwenyewe.'"

Katika hadithi nyingine iliyosimuliwa kutoka kwa Abu Huraira, tunakuta:

"Mwenyezi Mungu huwa anashuka mpaka kwenye mbingu ya kwanza, na ananyoosha mikono Yake miwili na anasema…"

"Vidole"

Hakuna utajo wa neno "vidole" ndani ya Qur'ani Tukufu kuhusiana na Mwenyezi Mungu; kwa hiyo, Ibn Khuzaimah alilazimika kutegemea juu ya hadithi pekee ili kuthibitisha kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa na vidole. Hadithi zenyewe hizo zinaweza kupatikana katika kitabu cha *Tawhiid* cha Ibn Khuzaimah, na ndani ya *Sahih Bukhari, Sahih Muslim*, *Sunan* ya Tirmidhi, *Sunan ibn Majah*, *Tafsir Tabari*, Ibn Kathiir na Suyuti pia. Hadithi moja kama hizo ni: Abdullah anasimulia kwamba kuhani mmoja (*rabbi*) alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akasema:
"Oh, Muhammad! Sisi tunasoma katika Taurati kwamba Allah anaiweka pepo katika kidole kimoja, miti yake katika kimoja, maji kwenye kingine kimoja, dunia na viumbe wote kwenye kimoja! Na halafu anasema: 'Mimi ndiye Mfalme!'

Mtukufu Mtume akatoa kicheko cha tabasamu kuthibitisha kile yule rabbi alichokisema, na katika kumuunga mkono maneno yake, akasoma Ayah ifuatayo:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ ۚ {67}

"Na hawakumheshimu Mwenyezi Mungu heshima ipasayo, na siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mkononi mwake na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kulia, …" (***Az-Zumar; 39: 67***)

Hadithi hizi kutoka kwa Abu Huraira na wengineo ziliwashawishi wanazuoni kutoka ile madhehebu kinyume na ya Ahlul-Bayt (a.s.) kutwaa ile maana halisi ya neno Yadullah popote linapotokea ndani ya Qur'ani Tukufu. Ibn Khuzaimah anao mlango mzima katika kitabu chake juu ya *Tawhiid*, ambao unasema:

"Uthibitisho kwamba Mwenyezi Mungu Muumba, Aliye Mkuu, anao mkono; kwa kweli Allah Aliye Mkuu anayo mikono miwili, kama tulivyojifunza kutoka kwenye Ayah madhubuti za Qur'ani Tukufu…"1

Halafu anaendelea kunukuu Ayah zifuatazo kwa ithibati ya madai yake:

وَقَالَتِ الْيَهُودُ يَدُ اللَّهِ مَغْلُولَةٌ ۚ غُلَّتْ أَيْدِيهِمْ وَلُعِنُوا بِمَا قَالُوا ۘ بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ يُنْفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ ۚ {64}

"Na Wayahudi walisema: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba. Mikono yao ndio iliyofumba, na wamelaaniwa kwa sababuya yale waliyoyasema. Lakini mikono ya Mwenyezi Mungu iwazi, hutoa apen- davyo ..." (***Al-Maida; 5: 64***)

فَسُبْحَانَ الَّذِي بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ {83}

"Basi ametakasika yule ambaye mkononi mwake umo ufalme wa kila kitu, na kwake mtarejea." (***Yaasin; 36: 83***)

قُلِ اللَّهُمَّ مَالِكَ الْمُلْكِ تُؤْتِي الْمُلْكَ مَنْ تَشَاءُ وَتَنْزِعُ الْمُلْكَ مِمَّنْ تَشَاءُ وَتُعِزُّ مَنْ تَشَاءُ وَتُذِلُّ مَنْ تَشَاءُ ۖ بِيَدِكَ الْخَيْرُ ۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ {26}

"Sema: Ewe Mola Mwenye kumiliki ufalme, humpa ufalme umtakaye, na humnyang'anya ufalme umtakaye. Na humtukuza yule umtakaye na kumdhalilisha umtakaye. Kheri yote imo mikononi mwako. Hakika wewe ni Mweza juu ya kila kitu." (***Aali Imraan; 3: 26***)

Hebu sasa tuelezee ni nini Madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) walichokisema.

Majibu Kutoka Kwa Ahlul-Bayt (A.S.)

(**a**) Muhammad bin Muslim alimuuliza Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) kuhusu Ayah ifuatayo:2

قَالَ يَا إِبْلِيسُ مَا مَنَعَكَ أَنْ تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ ۖ {75}

"Akasema: Ewe Iblis, ni nini kimekuzuia kumtii yule niliyemuumba kwa mikono yangu?.. (***Swaad; 38: 75***)

Imam Baqir (a.s.) akajibu:

“Yad (mkono) katika lugha ya Kiarabu linatumika kumaanisha uwezo na ukarimu.”

Halafu akaendelea na kutoa mifano zaidi kutoka kwenye Qur’ani Tukufu na fasihi ya Kiarabu ili kuonyesha ile tamathali ya usemi. Hapa tunanukuu baadhi ya mifano ambayo aliitoa:

وَاذْكُرْ عَبْدَنَا دَاوُودَ ذَا الْأَيْدِ ۖ إِنَّهُ أَوَّابٌ {17}

“…Na umkumbuke mja Wetu Daudi, mwenye mikono …” **(*Swaad; 38: 17*)**

Imam (a.s.) akaeleza kwamba katika Ayah hii, kule kutajwa kwa mikono ni dhahiri kabisa kwamba ni kwa kiistiari. Anachotaka kukifikisha Mwenyezi Mungu ni kwamba Yeye alimbariki Daudi na nguvu. Kisha yeye akaorodhesha mifano ya nguvu ambazo kwazo Daudi alibarikiwa kwazo:

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِأَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ {47}

“Na mbingu tumeiumba kwa mikono na hakika sisi ndio wapanuao” **(*Dhariyaat; 51: 47*)**

Imam (a.s.) akasema: “Hapa mikono inamaanisha uwezo.”

وَأَيَّدَهُمْ بِرُوحٍ مِنْهُ ۖ {22}

“… Na akawapa mkono kwa roho itokayo Kwake Mwenyewe…” **(*Al- Mujadilah; 58: 22*)**

Katika Ayah hii, “mkono” unaashiria kutia nguvu au uwezo. Akinukuu kutoka kwenye fasihi ya Kiarabu, Imam (a.s.) alisema: “Wanasema: Fulani wa fulani ana mikono mingi sana kwangu mimi.” Hii ina maana kwamba nina deni la shukurani kwake kwa sababu za wajibu.

Halafu tena, Waarabu wanao usemi wao: “Ana mkono mweupe juu yangu mimi!”

Hii ina maana kwamba amenifanyia hisani. Mikono katika muktadha huu unamaanisha ukarimu.

(b) Muhammad bin Ubaidah aliirejea Ayah hiyo hiyo ya Suratul-Swaad, kwa Imam ar-Ridha (a.s.). Majibu yalikuwa:

“Kwa Mikono Yangu” katika Ayah hii imekusudiwa kumaanisha “kwa nguvu na uwezo Wangu.”3

(c) Suleiman bin Marhan anasema kwamba yeye alimuuliza Imam Ja’far Sadiq (a.s.) kuhusu maana ya

ile Ayah ambamo Mwenyezi Mungu anatamka hivi:

وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ {67}

"...Na ardhi yote hiyo Siku ya Kiyama itakuwa mkononi mwake..." (***Az-Zumar; 39: 67***)

Imam (a.s.) akasema: "Ina maana ya udhibiti kamili na mamlaka yasiokuwa na mshirika yoyote."

Muhammad bin Ubaidah halafu akaendelea kuuliza kuhusu ile sehemu ya Ayah iliyokuwa imebakia: **"...Na mbingu zitakunjwa kwenye mkono wa kulia..."**

Imam (a.s.) akaelezea kama ifuatavyo:

"Mwenyezi Mungu amelitumia neno *Yamiin* ambalo linaashiria 'mkono,' na mkono una maana ya Ukarimu Wake na Uwezo. Hizo mbingu zitakunjwa kwa uwezo Wake."

Neno "ukufi" au "kulia Kwake" halimaanishi ngumi au mkono wa kulia.

Hayaashirii kwenye kiungo chochote kama inavyodhaniwa na madhehe- buya Makhalifa. Kudhania viungo na kuwepo kimwili kwa Mwenyezi Mungu ni kujiingiza kwenye shirki – na hiyo ndiyo iliyokuwa sababu kwa nini Imam Ja'far Sadiq (a.s.) baada ya kujibu swali hilo, alisisitiza juu ya kuimalizia Ayah hiyo. Yeye alisema:

سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ {67}

"Yeye ameepukana na upungufu na yu juu kabisa kuliko yale wanayomshirikisha nayo."[4] (***az-Zumar; 39: 67***)

Uchunguzi

Ahlul-Bayt (A.S.) wametegemeza hoja yao juu ya maana halisi ya Tawhiid, wakati huo huo, wakitegemea sana katika matumizi ya kawaida ya neno hilo miongoni mwa Waarabu na katika fasihi yao. Raghib Isfahani ndani ya kitabu chake mashuhuri, *Mufradatul Qur'an* anasema:

"***Yad*** lina maana ya 'mkono,' ambao ni kiungo. Lakini lina maana nyingine vile vile kama: udhibiti, uwezo na busara."

Wanazuoni wa Misri wameorodhesha maana tisa tofauti juu ya neno Yad, mbali na ile ya mkono. Kwa mfano, Ayah ifuatayo:

فَسُبْحَانَ الَّذِي بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ {83}

“Basi ametakasika yule ambaye mkononi mwake umo ufalme wa kila kitu… **(*Yaasin; 36: 83*)**

inatafsiriwa kama: “Ambaye katika udhibiti wake kamili ndimo ulimo umiliki juu ya vitu vyote.”

Jambo la kushangaza kabisa ni kwamba wanazuoni hawa ambao wamehusisha mikono na viungo vingine kwa Mwenyezi Mungu wakati wakifasiri Ayah zinazohusika, walitwaa msimamo mwingine pale neno hilo lilipotumika kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Katika Ayah ifuatayo, iliyozungumzwa kwa Mtume (s.a.w.w.), watarjuma na wafasiri wote wanakubaliana kwamba lina maana:

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ {29}

“Wala usiufanye mkono wako* (*kama*) *uliofungwa shingoni mwako* (*kwa ubakhili*)*..”
(*Bani Israil; 17: 29*)

Hakuna hata mmoja miongoni mwao aliyelichukulia hilo neno ‘mkono’ kwa maana halisi. Lakini ilipokuja kwenye neno hilo hilo kutumiwa juu ya Mwenyezi Mungu, wao walikimbilia kwenye maana yake halisi, wakipuuza kabisa ile ya kiistiari.

Hii inajulisha ile athari kubwa iliyotawaliwa na dhana za Kiyahudi na Kikristo, ambazo ziliimarishwa bila majuto na masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) wasiokuwa na maadili. Habari hizi haziishii hapa. Kuna maelezo ya kuvutia yanayofuata bado.

Mlango Wa Tano: Nyayo Za Mwenyezi Mungu

“Nyayo Za Mwenyezi Mungu” Na “Muundi Na Mguu” Wake!!”

Katika kitabu cha *Tawhiid* cha Ibn Khuzaimah, hadithi mbalimbali zinazohusiana na ‘mguu’ na ‘nyayo’ za Mwenyezi Mungu zimetajwa humo, aghalabu zikisimuliwa na Abu Huraira. Na zinaweza kupatikana vilevile katika *Sahih Bukhari, Sahih Muslim, Sunan Tirmidhi, Musnad Ahmad Hanbal* na *Tafsiir* za akina Tabari, Ibn Kathiir na Suyuti.
Abu Huraira anasimulia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

“Pepo na Jahannam zilikuwa na mzozo, kila kimoja kikijaribu kuonyesha ule ubora wake juu ya kingine.” Basi Jahannam ikazungumza: “Mimi nimependelewa kwa kuwepo kwa wale watu wenye kiburi na nguvu ndani yangu.” Pepo ikajibu: “Mimi sijui ni kwa nini hakuna mtu isipokuwa wale dhaifu na wanyenyekevu

ndio walioingizwa ndani yangu!”

Hivyo Mwenyezi Mungu akaiambia Pepo:

“Wewe ndiye Msamaha Wangu, na kupitia kwako ninatoa msamaha kwa yeyote kati ya waja Wangu.”

Halafu Yeye akazungumza na Jahannam:

“Wewe ndio ghadhabu Yangu, na kupitia kwako wewe ninamuadhibu yeyote nitakaye kumuadhibu. Kila mmoja wenu atajaa.”

“Bali Jahannam haitajaa, hivyo Mwenyezi Mungu ataingiza mguu Wake ndani yake.”

Kisha Jahannam itagutia:

“Tosha! Inatosha!”

Hivyo kwa njia hii Jahannam itajaa, kwani Mwenyezi Mungu hamdhulumu yoyote yule. Na kuhusu hiyo Pepo, Yeye ataumba upya kwa maalum kabisa viumbe wa kuifanya ijae.

Huo “Muundi” Au “Mguu”

Ndani ya Sahih Bukhari, Mustadrak ya Hakim, Tafsiir za Tabari, Ibn Kathiir na Suyuti, tunazikuta hadithi zinazoshughulika na ‘muundi’ wa Mwenyezi Mungu. Katika Ayah ifuatayo:

يَوْمَ يُكْشَفُ عَنْ سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ {42}

“Siku ambayo ‘Shin’ (muundi) zitakapowekwa wazi (itakaposhuka adhabu), na wataitwa kusujudu lakini hawataweza.” (Al-Qalam; 68:42)

Abu Saeed, sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema yeye alimsikia Mtume akisema:

“Mola Wetu atakujaweka wazi muundi Wake, kisha kila muumini mwanaume na mwanamke atapiga magoti mbele Yake, isipokuwa wale ambao walimuabudu katika ardhi ili kujionyesha au kuwapendezesha watu wengine – wao hawataweza kuinama, na watabakia wima.”

Hadithi hii imepewa utendewaji wa kina na Bukhari katika ule Mlango juu ya Tawhiid; tunanukuu hapa baadhi ya dondoo:

“Itakuja kutangazwa hiyo Siku ya Kiyama: ‘Kila mmoja wenu asimame mstari nyuma ya miungu mliyokuwa mkiiabudia. Hivyo watu watakimbilia kufanya vikundi nyuma ya miungu yao, isipokuwa wale waliomuabudu Mwenyezi Mungu ndio watakaobakia imara juu ya uwanja wakimsubiri Yeye.’

“Halafu Mwenyezi Mungu atatokea na atawauliza: ‘Je, mlikuwa na dalili au ishara yoyote yenye kutambulisha kati ya Mwenyezi Mungu na nyie wenyewe ambayo itawawezesha ninyi kumtambua Yeye?’

“Wao watasema: ‘Ndiyo! Ule Muundi.’

Kisha Mwenyezi Mungu ataudhihirisha muundi Wake, ambao baada ya kuuona huo wale waumini watasujudu na watamfuata hadi Peponi.”

Maswali mengi ya kushangaza yanachipuka kwenye akili zetu baada ya kusoma hadithi hiyo hapo juu:

a) Ni nini asili ya hii ‘dalili’ au ‘ishara’ ya utambuzi inayowakilishwa na hii inayodaiwa kuwa muundi au mguu wa Mwenyezi Mungu?

b) Ni lini ambapo wanazuoni wa madhehebu ya Makhalifa walipouona huo muundi kwa mara ya kwanza, kiasi kwamba wao wanategemea kuja kuutambua hiyo Siku ya Kiyama kama dalili?

c) Na kama waliuona hapa duniani, ulikuwaje, unafananaje?

d) Ulikuwa wa ukubwa gani?

Maelezo Kutoka Kwenye Madhehebu Ya Ahlul-Bayt (A.S.)

Hebu natuchukue Ayah ifuatayo:

يَوْمَ يُكْشَفُ عَنْ سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ {42}

“Siku hiyo ambayo muundi utakapowekwa wazi (itakaposhuka adhabu), na wataitwa kusujudu lakini hawataweza.” **(*Al-Qalam; 68:42*)**

Ubaidah ibn Zararah anasema:

“Nilimuuliza Imam Ja’far as-Sadiq (a.s.) kuhusu Ayah hii. Yeye mara moja akaweka mkono wake juu ya kifundo cha mguu, akiiondoa ile nguo juu yake, na akaweka mkono wake juu ya kichwa chake akisema: ‘Sifa zimwendee Allah Ambaye ni Mkuu aliye Juu.’”

Sheikh Saduuq anasema kwamba madhumuni ya kufanya hivyo ilikuwa ni kujulisha kwamba Mwenyezi Mungu, Aliye Mtukufu, ni zaidi na yu mbali na kuwa mwenye mguu au muundi.

Sahaba mwingine wa Imam (A.S.) aliyeitwa Muhammad ibn Ali Halabi aliuliza kuhusu uwekwaji wazi wa huo muundi. Safari hii Imam alitoa jibu lenye maelezo mafupi. Alisema:

“Ametukuka yule Mwenye Uwezo, (Mwenyezi Mungu)”

Halafu aliisoma Ayah hiyo nzima, pamoja na ile Ayah inayofuatia mara tu:

يَوْمَ يُكْشَفُ عَنْ سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ {42}

خَاشِعَةً أَبْصَارُهُمْ تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ۖ وَقَدْ كَانُوا يُدْعَوْنَ إِلَى السُّجُودِ وَهُمْ سَالِمُونَ {43}

“…na wataitwa kusujudu lakini hawataweza. Macho yao yatainamishwa chini, unyonge utawafunika, na hakika walikuwa wakiitwa kusujudu walipokuwa salama.” **(*Al-Qalam; 68: 42-43*)**

Imam (a.s.) akasema:

“Kifungu hiki cha maneno ni cha kiistiari kilichotumika kwa nyakati ngumu sana na zenye mitihani. Kinaelezea jinsi watu fulani katika Siku ya Kiyama watakavyokuwa wamefunikizwa na aibu na fedheha, wakiwa hawana cha kusingizia. Ayah hizi, wakati zinaposomwa kwa pamoja, zinaielezea ile istiari.”

Sheikh Saduuq ndani ya kitabu chake juu ya Tawhiid anafafanua zaidi:

“Pale Imam (a.s.) aliposema: ‘Ametukuka yule Mwenye Uwezo (Mwenyezi Mungu), na kisha akaondoa ile nguo iliyofunika muundi wake, iliashiria kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa mbali na kuwa na kiungo chochote! Maneno ‘kuacha muundi wazi’ yasichukuliwe kwa maana yake halisi.”

“Kuacha Muundi Wazi” Kama Ilivyotumika Kwenye Fasihi Ya Kiarabu.

Abdullah ibn Abbas, yule binamu yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema:
“Wakati wowote unapokuwa huwezi kuielewa Qur’ani, tafuta ufafanuzi kutoka kwenye fasihi ya Kiarabu. Humo katika matumizi yake, unaweza ukaipata maana yenyewe. Je, hukumsikia yule mshairi wa Kiarabu aliyesema: *Qamatil Harbu Bina Ala Saqin* – ‘Vita vimeanza pamoja na makali yake na matatizo…’”

Hivyo ‘kuachwa wazi kwa muundi’ katika Ayah hii kumeelezea hofu kubwa, aibu na fedheha ambayo itajiri katika siku hiyo.5

Raghib Isfahani katika kitabu chake maarufu, *Mufradat al-Qur’an* ametoa maana hiyo hiyo kwenye Ayah hii, kama alivyoieleza Ibn Abbas. Vivyo hivyo, wanazuoni wa Ki-Misri wameiunga mkono ile fasiri ndani ya *Mu’jam Alfadh al-Qur’an al-Karim.*

Ni dhahiri kabisa, ile tamathali ilikuwa ikifahamika vema miongoni mwa Waarabu na wanazuoni wao kwa karne kumi na nne zilizopita. Cha kuhuzunisha sana, Madhehebu ya Makhalifa imechagua kukubaliana na hadithi za Abu Huraira na wale wa aina yake, wanaohusisha viungo na kano kwa Mwenyezi Mungu.

Kitenzi kilichotumika ndani ya Ayah hii ni cha kauli ya kutendwa; ambayo ina maana:

“Itakuja kuachwa wazi…”

Bado tunawakuta wanazuoni wao wakikitwaa kitenzi hicho katika kauli tendi, hivyo kupata tafsiri hii:

“Mwenyezi Mungu atakuja kuacha muundi Wake wazi.”

Kwa kuhitimisha, tunasema:

1. Madhehebu hii, ambayo ilijitenga na Ahlul–Bayt (a.s.) imeitafsiri vibaya Qur’ani Tukufu.

2. Wamehusisha hadithi bandia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

3. Wameanzisha uhusishaji wa viungo kwa Mwenyezi Mungu miongoni mwa Waislamu.

Tunapaswa kuwashukuru Ahlul–Bayt (a.s.) daima ambao wamejaribu, mbali na tofauti zote, kuhifadha usafi wa Uislamu, na pia kuhifadhi maana halisi ya Qur’ani Tukufu na Hadith.

Sifa zote zimwendee Mwenyezi Mungu! Tunajua sasa kwamba Mwenyezi Mungu hana umbile, wala mwili. Yeye hana viungo, hahitaji chochote kati ya hivyo. Kwani kama angekuwa na mwili, angepaswa kuwa na makazi! Hebu sasa tuchunguze shimo la ziada ambamo madhehebu ya Makhalifa imeangukia.

---

1. Tawhiid, cha Ibn Khuzaimah – uk. 53
2. Tawhiid, cha Saduuq – uk.153
3. Tawhiid, cha as–Saduuq, uk. 153–154
4. Tawhiid, cha Saduuq – uk. 160–161.
5. Tafsiir ya Suyuti – Juz. 6, uk. 254

Sura Ya Sita: Kiti Cha Enzi Cha Mwenyezi Mungu

“Kiti Cha Enzi” (Arshi) Na “Kiti” (Kursiyu) Inavyofahamika Kwa Madhehebu Ya Makhalifa:

Bila shaka, kwa mujibu wa Madhehebu ya Makhalifa, Mwenyezi Mungu lazima awe ana makazi! Wakiwa wamemfikiria kuwa kama mwanadamu mwenye umbile, na viungo, basi wanapaswa kumpatia sehemu, ambayo itaupatia mwili huo nafasi ya kuishi. Hivyo, tunamkuta yule kiongozi wa ushirikishaji mwili kwa Mwenyezi Mungu, Muhammad ibn Uthman Darami (aliyefariki mnamo mwaka 280 Hijiria) akiandika katika kitabu chake, *al-Radd ala al-Jahmiyyah,* kwamba:

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu anacho Kiti cha enzi kinachotambulika na kinachoelezeka juu ya mbingu ya saba, kinachobebwa na Malaika. Mwenyezi Mungu, kama ambavyo Yeye alivyojieleza Mwenyewe, hafanani na viumbe vyake.”

Halafu anaendelea katika mlango wa kumi na tatu wa kitabu hicho hicho, chini ya kichwa cha maneno:

“Kujiweka imara kwa Mola, Mtukufu, juu ya Arshi, kujinyanyua Kwake kwenye mbingu na kuwa Kwake tofauti na viumbe vyake.”

Vivyo hivyo, Ibn Khuzaimah anao mlango ndani ya kitabu chake cha Tawhiid uitwao:

“Kujiweka imara kwa Muumbaji wetu, aliye Mtukufu, Muweza, juu ya Kiti Chake, na kuwa juu yake na juu ya yote.”

Katika hoja ya kuvutia sana iliyotolewa na Darami, tunamkuta yeye kwa ushupavu sana akiwakanusha wale wanaoamini kwamba Mwenyezi Mungu yupo kila mahali. Yeye ananukuu hadithi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

“Mbegu ya uzazi inabakia ndani ya tumbo la uzazi kwa muda wa usiku wa siku arobaini, na halafu malaika anayehusika na roho za watu anapanda nayo kwa Mola na kuuliza: ‘Ewe Mungu Wangu! Je, mja wako huyu amepangiwa kuwa mwanaume au mwanamke…?’”

Halafu Darami anasema:

“Kama ukweli ungekuwa kama unavyoamini, basi Mwenyezi Mungu angekuwa ndani ya tumbo pamoja na ile mbegu. Kama ni hivyo, kulikuwa na haja gani ya malaika kupaa pamoja na ile mbegu?”

Zaidi ya hayo, yeye anaongezea:

“Mwenyezi Mungu yupo na anaishi kwa kujitenga na viumbe Vyake. Kwa nini ajitafutie Mwenyewe makazi kwenye sehemu chafu, ndani ya matumbo ya wanadamu, ndege na wanyama? Kwa nini kila upenu na pembe iwe Naye ndani yake?”

Darami, Ibn Khuzaimah na wanazuoni wengine kutoka Madhehebu ya Makhalifa wanahakikisha imani

zao kuhusu “Arshi” au “Kiti” halisi cha Mwenyezi Mungu kutoka kwenye Ayah nyingi za Qur’ani Tukufu na hadithi. Hapa ni baadhi ya mifano:

“Arshi” Na “Kursiyu” Kama Inavyoeleweka Kwenye Madhehebu Ya Makhalifa:

Bukhari, Tirmidhi, Ibn Majah, Ahmad Hanbal, Tabari, Ibn Kathiir na Suyuti wamenakili yafuatayo katika vitabu vyao vikuu:

“Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliulizwa: ‘Mwenyezi Mungu alikuwa amekaa wapi kabla Hajauumba ulimwengu?’ Yeye akajibu akisema: ‘Alikuwa katikati ya giza, mawingu mazito – yasiyokuwa na upepo chini yake wala juu yake. Na hapakuwa na kiumbe kingine. “Arshi” Yake ilikuwa ikielea juu ya maji.’”

Wanazuoni hawa wameifasiri Ayah ifuatayo: **“Na Arshi Yake ilikuwa juu ya maji…”** (***Huud; 11: 7***) kama kiti cha kimaada kilichowekwa juu ya maji. Katika ufafanuzi zaidi, wao wanaendelea kunukuu hadithi ya kuchukiza ifuatayo:

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Umbali baina ya ardhi na mbingu ni miaka sabini na moja, sabini na mbili au sabini na tatu. Na huo huo ndio umbali kati ya mbingu ya pili na ya tatu, vivyo hivyo, mpaka ya saba. Na juu ya mbingu ya saba ni bahari ambayo kina chake ni kipimo cha umbali kati ya mbingu mbili. Juu ya bahari hiyo kuna mbuzi wa mlimani wanane, kwato na magoti yao vimeachana kama umbali baina ya mbingu mbili. Juu ya migongo yao ni ile Arshi kubwa ya Mwenyezi Mungu ambayo urefu wake ni sawa na umbali baina ya mbingu mbili. Hapo, juu yake amekaa Mwenyezi Mungu, Mtukufu na Mkuu.”1

“Arshi” Yenye Kugongagonga.

Soma hadithi ifuatayo kutoka kwa Ibn Khuzaimah, Abu Dawuud, Ibn Athiir na Aaluusi na utabasamu! Hadithi yenyewe inasema kwamba wakati mmoja Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikutanisha vidole vyake kufanya umbo la kuba na akasema:

“Arshi ya Mwenyezi Mungu, juu ya mbingu zote, ni kama hivi. Na inachacharisha na kugongagonga kama mgongano wa matandiko ya ngamia wakati mtu anapompanda juu yake.”

Abu Dawuud katika Sunan yake, anasimulia kutoka kwa Basshar, hadithi ifuatayo:
“Mwenyezi Mungu amekaa kwenye Arshi Yake, na Arshi hiyo iko juu ya mbingu. Na Arshi hiyo inatoa makelele chini Yake, kwa namna ile matandiko ya ngamia yanavyogongana wakati mtu anapompanda.”

Tabari, Ibn Kathiir na Suyuti wanasimulia hadithi ifuatayo ndani ya Tafsiir zao kutoka kwa Khalifa Umar: Mwanamke mmoja wakati fulani alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akasihi:

“Niombee ili niweze kuwa miongoni mwa wale watakaoingia Peponi.” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akalitukuza jina la Mwenyezi Mungu na halafu akasema: “Kiti cha Mwenyezi Mungu kina ukubwa sawa na mbingu na ardhi na kinapiga makelele chini ya uzito Wake kama tandiko jipya la ngamia chini ya uzito wa mtu. Na Anakizidi kiti hicho pande zote kwa urefu wa vidole vinne!!’”

Vema, huyo ni Mwenyezi Mungu, mnene mno kiasi kwamba haenei katika “Arshi” Yake – Mwenyezi Mungu atuepushe na imani chushi kama hiyo. Sasa hebu tukichunguze chanzo chake.

Hadithi Ya Ka’b Al-Ahbar

Yeye anasema:

“Mwenyezi Mungu aliziumba mbingu saba, na ardhi pia kama hizo mbingu; na halafu akaziweka mbingu hizo kila moja mbali na nyingine, kipimo kile kile kama kile baina ya ardhi na mbingu ya dunia, na akazifanya kuwa nzito. Halafu akakinyanyua Kiti Chake juu ya mbingu hizo na akajiweka Mwenyewe juu yake.

Hivyo kila mbingu miongoni mwa mbingu hizo inapiga makelele na kugongagonga kutokana na uzito wa Mwenyezi Mungu, kwa namna ile kama tandiko jipya la ngamia linavyopiga kelele wakati mpandaji akikaa juu yake kwa mara ya kwanza.”

Hiki ndio chanzo chenyewe. Alikuwa ni Ka’b al-Ahbar, aliyekuwa Rabbi hapo mwanzoni, ambaye alianzisha upuuzi huu kwenye wingi wa hadithi za Kiislamu na akazihusisha kwa uongo na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

“Kursiy” Ni Nini, Na Ni Nani Wabebaji Wake

Ndani ya Tafsiir yake, Maqatil anaelezea Ayah ifuatayo kutoka ndani ya Qur’ani Tukufu:

وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ {255}

“…Na kiti chake kimeenea mbingu na nchi …” (***Al-Baqarah; 2: 255***)

Yeye anasema:

“Hiyo “Arshi” au “Kiti” kimebebwa na Malaika wanne:

Mmoja ana uso wa binadamu, na anaomba kwa ajili ya riziki juu ya wanadamu.

Wa pili anayo sura ya mnyama, kama ile ya dume la ng’ombe. Anaomba kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya riziki ya wanyama.

Malaika wa tatu anafanana na tai, akiwakilisha ndege. Yeye anawaombea ndege.

Huyo wa nne ni kama simba, akiwakilisha wanyama wa mwituni, na anawaombea riziki yao.”2

Hadithi kutoka Madhehebu ya Makhalifa zinahuzunisha kwa visa vya njama na uwongo kama hizi. Zaidi ya hayo, ni hapo tutakapokuwa tukielezea imani zao kuhusu kuhudhuria kwa Mwenyezi Mungu katika hiyo Siku ya Kiyama.

Ibn Khuzaimah katika kitabu chake juu ya Tawhiid amenukuu Ayah za Qur’ani Tukufu zifuatazo, ili kuthibitisha kwamba Mwenyezi Mungu Mwenyewe ametudhihirishia sisi juu ya makazi Yake!

الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ {5}

“Mwenyezi Mungu amejiimarisha juu ya Arshi…” (***Twaha; 20: 5***)

ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۖ {59}

“Kisha akajiimarisha Mwenyewe juu ya Arshi…” (***Furqan; 25: 59***)

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ {7}

“Ni Yeye ambaye ameziumba mbingu na ardhi katika siku sita na Arshi Yake ilikuwa juu ya maji…..” (***Huud; 11: 7***)

Ibn Khuzaimah anaamini kwamba Ayah hizi zinaashiria kwenye moja ya fanicha anayoitumia Mwenyezi Mungu kama kiti Chake! Na yeye hayuko peke yake. Wanazuoni wengi wamefuata nyayo zake, wakisahau kwamba maneno haya yametumiwa kiistiari kuelezea ufalme na mamlaka.

Madhehebu Ya Ahlul-Bayt (A.S.)

Imam Ja’far Sadiq (a.s.) aliulizwa kuhusu Ayah ifuatayo:

وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ {255}

"...Na kiti chake kimeenea mbingu na nchi ....." **(*Al-Baqarah; 2: 255*)**

Yeye (a.s.) akasema: "Kursiyu" inaashiria elimu Yake na Ayah hii ina maana:

'Elimu yake imezienea mbingu na ardhi.'"

Katika hadithi nyingine kutoka kwa Imam Ja'far Sadiq (a.s.) tunayakuta maneno yafuatayo:

"Mbingu na ardhi vyote vimo kwenye 'Kursiy' Yake,'3 yaani elimu."

Mtu mwingine alikuja kwa Imam Ja'far Sadiq (a.s.) akiomba maelezo juu ya "Arshi juu ya maji."

Imam (a.s.) akauliza: "Wao wanasema nini?"

Yule mtu akasema: "Wanasema kwamba Arshi ya Mwenyezi Mungu iko juu ya maji, na Yeye amekaa juu yake."

Imam (a.s.) akasema:

"Kwa hakika huo ni uwongo! Yeyote anayeamini kwamba Mwenyezi Mungu anakadirika na anabebwa, anamfanan- isha na viumbe! Na kile ambacho kinazuia au kinabeba lazima kiwe na nguvu zaidi Yake!"

Yule mtu aliduwaa na kuwa kimya kwa muda kiasi na halafu akasema: "Ninaweza kuwa fidia yako? Naomba nijifunze kutoka kwako, ile maana halisi."

Imam (a.s.) akasema:

"Ndani ya Ayah mbalimbali za Qur'ani Tukufu, hili neon 'Arsh' limekuja katika muktadha mbalimbali. Maana yake katika kila suala ni ama 'ufalme' au 'mamlaka' au 'elimu.'"
Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَهُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ {129}

"Mola wa 'Arshi' Kuu." **(*at-Tawbah; 9: 129*)**

Hapa utukufu wa Mwenyezi Mungu unawakilishwa katika neno 'Arshi', ambalo ni Ufalme Wake.

Katika Ayah nyingine

الرَّحْمَٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَىٰ {5}

"Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema amjiimarisha juu ya 'Arshi'....." **(*Twaha; 20: 5*)**

Maana yake ni kwamba mamlaka Yake yameenea kwenye ufalme Wake. Na pale Mwenyezi Mungu anaposema: **"Arshi Yake ilikuwa juu ya maji,**

Yeye ana maana kwamba maji yaliumbwa kabla ya mbingu na ardhi, na yalikuwa ndio kiumbe cha kwanza kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu." Kwa kweli, Ibn Khuzaimah na wale wanaofanana naye wamepotoshwa na lile neno *Istawaa* ambalo limetokea ndani ya Qur'ani Tukufu pamoja na 'Arsh'. Wao wamelitafsiri kwa maana halisi kama "amekaa" au "ametulia." Ndani ya Qur'ani, tunakuta Ayah sita ambamo neno hilo limetumika. Raghib Isfahani anasema ndani ya Tafsiri yake:

"Kila wakati hiki kitenzi *Istawaa* kinapogeuzwa kwenye hali elekezi pamoja na 'Ala,' inamaanisha *Istiila* – udhibiti, kujitwalia, ushindi, uwezo, kama ndani ya Ayah: 'Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema anao udhibiti kamili juu ya 'Arsh.'"

Hali kadhalika, tunalikuta neno hilo likiwa limetumika katika fasihi ya Kiarabu kwa kidokezo hicho hicho. Mshairi mmoja anamsifia Bushr bin Marwan, ndugu yake yule Khalifa wa Bani Umayyah, Abdul Malik, katika ubeti ufuatao:

"Bushr ameiteka Iraq bila ya kushika na kutumia upanga au kumwaga damu yoyote..."(*Qad istawaa alal Iraqi...*)

Neno jingine, ambalo limeleta matatizo – juu ya madhehebu ya Makhalifa yenye kushirikisha viungo kwa Mwenyezi Mungu, ni **Kursyu.** Wao wamelichukulia kwa maana halisi, likimaanisha kigoda au kiti. Tabari ndani ya *Tafsiir* yake anasema kwamba *Kursiyy* inamaanisha elimu pia, na ni kwa sababu hii kwamba vitabu vya elimu vinaitwa *Kurrasah*, na watu waliosoma hasa wanaitwa *Kurasiyy*. Qur'ani Tukufu imelibadilisha neno Kursiyy na neno Ilm ndani ya Ayah kadhaa, ambazo zinazungumza katika mwelekeo mmoja. Kwa mfano:

وَسِعَ رَبِّي كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ۚ {80}

"...Mola Wangu anao wasaa wa elimu juu ya kila kitu ..." **(*Al-An'aam; 6: 80*)**

وَسِعَ رَبُّنَا كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ۚ {89}

"...Mola Wetu amekienea kila kitu kwa elimu..." **(*Al-A'araf; 7: 89*)**

رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَحْمَةً وَعِلْمًا {7}

***"Mola Wetu! Wewe umevienea vitu vyote kwa huruma na elimu."* (*Al- Mu'min; 40: 7*)**

إِنَّمَا إِلَٰهُكُمُ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ وَسِعَ كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا {98}

***"Hakika Mola Wenu ni Mwenyezi Mungu mmoja tu, ambaye hakuna aabudiwaye ila Yeye tu, anakijua kila kitu kwa elimu* (*Yake*)*."* (*Twaaha; 20: 98*)**

Katika Ayah zilizotangulia, kitenzi '**wasia**' kimetumika pamoja na '**Ilm.**' Hata katika ile Ayah pekee ambamo **Kursiyy** imetumika, inavutia kuona kwamba kipande cha Ayah hiyo kilichotangulia kinazungumzia juu ya elimu ya Mwenyezi Mungu pana na yenye kuenea. Hebu tuichunguze Ayah hiyo kama inavyoanza:

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۖ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ ۚ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۖ {255}

***"Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao – wala wao hawajui kitu katika elimu yake ila kile apendacho yeye. Elimu* (*Kursiy*) *yake imeenea mbingu na nchi..."* (*Al-Baqarah; 2: 255*)**

Mukhtasari

Kwa mujibu wa Madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.), kwa hiyo, **Arsh** na **Kursiyy** yanaashiria ufalme, mamlaka na elimu. Matumizi ya maneno haya ni ya kiistiari. Hili ni kinyume kabisa na kile ambacho madhehebu ya upande wa pili ilivyoongozwa kuamini kwa sababu ya athari za Kiyahudi.

---

1. Sunan Abu Dawuud – Juz. 4, uk. 231; Sunan Ibn Majah, Juz. 1, uk. 69; Musnad ya Ahmad Hanbal, Juz. 1, uk. 207.
2. Tafsiir Maqatil, Juz. 1, uk. 122.
3. Tawhiid, cha Saduuq – uk. 327-328.

Sura Ya Saba: Makazi Ya Mwenyezi Mungu

Washirikishaji Viungo Kwa Mwenyezi Mungu Miongoni Mwa Waislamu:

Madhehebu hii, ingawa ni kongwe, ya siku nyingi, ina ngome juu ya Waislamu wenye imani halisi, hususan ***Wahabia***. Ni muhimu kufanya uchuguzi mfupi wa imani zao na halafu tuzilinganishe na mafundisho ya Ahlul–Bayt (a.s.)

Kwa vile walihusisha sifa zote za mwanadamu kwa Mwenyezi Mungu, wao hatimae walilazimika kubuni sehemu kwa ajili Yake. Na baadae, waliikuza dhana, ambayo ilipiga taswira ya mabadiliko kichwani,uhamaji na kubadili maskani kwa Mwenyezi Mungu.

(I)Abu Huraira Anasimulia Kutoka Kwa Mtukufu Mtume (S.A.W.W.) “

Katika sehemu ya usiku, au labda katika theluthi ya mwisho ya usiku, Mwenyezi Mungu anashuka hadi kwenye mbingu ya kwanza na anatangaza: ‘Kuna mtu yoyote atakayeniita ili niweze kujibu maombi yake, anayeniomba mimi ili niweze kumpa? Ni nani atamkopesha Yule Ambaye Anajitosheleza na Muadilifu?’”1

(II) Katika Hadithi Nyingine Kutoka Kwa Abu Huraira, Haruun Bin Said Ameongezea:

“Halafu Mwenyezi Mungu ananyoosha mikono Yake na anasema: ‘Ni nani atakayetanguliza mkopo kwa Yule Ambaye hana shida wala sio dhalimu.’”2

Bukhari amesimulia pia hadithi kama hizo kutoka kwa Abu Huraira ndani ya mlango wake juu ya *Tawhiid, Da’awwat* na *Tahajjud*. Tena hayuko peke yake. Ameungwa mkono na Ibn Majah, Tirmidhi na Abu Dawuud, ambao wote wamesimulia hadithi zilizokusudiwa kuthibitisha kwamba Mwenyezi Mungu anashuka kimwili kwenda chini na juu ya mbingu!

(III) Ibn Khuzaimah Anasimulia Kutoka Kwa Abu Huraira

“Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: ‘Malaika wanakusanyika wakati wa Swala ya Asubuhi na Jioni.

Wale wa usiku wanapanda na wale wa mchana wanabakia. Na halafu Mwenyezi Mungu anawauliza wale Malaika
wa usiku:

‘Waja Wangu walikuwa katika hali gani wakati mlipowaacha?’ Malaika hao wanasema: ‘Tuliwashukia juu yao wakati wakiwa wanaswali, na tuliwaacha wakiwa wanaswali.’”

Akitoa maoni juu ya hadithi hii, Ibn Khuzaimah anaongezea: “Hadithi hii kwa uwazi kabisa inajulisha kwamba Mwenyezi Mungu yuko juu mbinguni, na kwa hiyo, Malaika wanasafiri kutoka ardhini kwenda juu mpaka Kwake. Wale (jahmiyyah) wanaoamini Mwenyezi Mungu yuko mbinguni na katika ardhi vile vile ni waongo, kwa sababu kama ingekuwa ni hivyo, basi Malaika wangemwendea juu ya ardhi au mahali penginepo katika tabaka za chini za dunia. Mwenyezi Mungu awalaani Jahmiyyah daima milele!”

Darami anaiunga mkono dhana hiyo, akitegemeza hoja yake juu ya neno *Nazala* (kwa maana halisi ikiwa ni ‘kushusha chini’) lililotumika kwa ajili ya Qur’ani Tukufu – yeye anasema:

“Ayah kama hii zinaweza kupatikana ndani ya Qur’ani kati- ka sehemu nyingi. Zote kwa uwazi kabisa zikieleza kwam- ba Mwenyezi Mungu aliishusha Qur’ani Tukufu kutoka huko juu mbinguni. Ingekuwa ni kwa namna wanavyoamini kwamba Mwenyezi Mungu yupo kila mahali, juu ya ardhi na chini yake, basi Yeye angesema: “Tumeitoa,” au “Tumeinyanyua” Qur’ani. Ayah hizo ziko wazi katika kutangaza mahali pa Mwenyezi Mungu paliponyanyuka, na haihitaji kufasiri zaidi.”3

Darami anaelekea kuwa mwenye kujawa na imani yake kwamba Mwenyezi Mungu amezuilika kwenye sehemu Yake katika mbingu.

Akizungumzia safari ya mbinguni ya Mtukufu Mtume wetu (s.a.w.w.) – *Mi’raj* – yeye anasema:

“Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwasimulia waumini matukio yake ya wakati wa kupaa kwake, jinsi alivyochukuliwa kutoka mbingu moja hadi nyingine, hadi ile ya mbali juu kabisa karibu na *Sidratul Muntaha* (kwa maana halisi ikiwa ni mti ulioko mbinguni). Ikiwa hicho wanachoamini wapin- zani ni kweli, kwamba Mwenyezi Mungu yupo kila mahali, basi kulikuwa na haja gani ya Buraq na huko kupaishwa? Kwa nini Mtume (s.a.w.w.) alipelekwa mbinguni, na kwa nani? Mnashikilia kwamba Mwenyezi Mungu yuko kila mahali, hata ndani ya nyumba ya Mtume (s.a.w.w.), bila hata ya pazia hapo katikati. Hivyo kwa nini kwenda huko juu?”

Madhehebu Ya Ahlul-Bayt (A.S.) Inaelezea:

Suala la kuhama na kubadili sehemu au kupanda juu na kushuka, kuhusiana na Mwenyezi Mungu ni jambo lisilopasika kabisa. Madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) inasema kwamba tabia kama hizo zinahusika kwa yule aliyeumbwa na sio kwa Muumba, Ambaye ni Mwenye kudra.

Imam ar-Ridha (a.s.) aliliweka wazi kabisa wakati alipoulizwa kuhusu Ayah ifuatayo:

وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا {22}

“Na akaja Mola Wako na Malaika safu kwa safu.” (***Fajr; 89: 22***)

Yeye (a.s.) akasema:

“Mwenyezi Mungu hawezi kuelezewa kwa namna ya mwendo, kuwasili, kuondoka, kuonekana na kutokuwepo. Yeye yuko zaidi na yu mbali na matukio kama hayo. Ayah inayohusika inaonyesha utaratibu wa Mwenyezi Mungu na amri Zake ambazo baadae zitadhihirishwa.”4

Seyyid Abdul Adhiim al-Hasani anasimulia kutoka kwa Ibrahim bin Abi Mahmud kwamba yeye alimuuliza Imam ar-Ridha (a.s.) kuhusu ile hadithi mashuhuri ambayo inazungumzia juu ya kushuka chini kwa Mwenyezi Mungu kila usiku hadi kwenye mbingu ya chini kabisa. Imam (a.s.) akasema:

“Ewe Mola Wangu walaani wale wanaoyahamisha yale maneno matakatifu kutoka mahali pao pale panapostahiki! Wallahi! Mtume (s.a.w.w.) hakusema kwa namna wao wanavyosimulia. Kile yeye alichokisema ni kwamba:

‘Mwenyezi Mungu Mtukufu huamuru Malaika kushuka chini hadi kwenye mbingu ya chini kabisa katika theluthi ya mwisho ya kila usiku, na kila Ijumaa usiku, katika theluthi yake ya kwanza.
Halafu Anamuamuru Malaika huyo kutangaza:

“Je kuna yoyote mwenye kuomba ili niweze kumpa? Yeyote mwenye kutubia ili niweze kumuwia radhi? Yeyote anayeomba msamaha ili niweze kumsamehe? Ee, yule anayeomba wema, jitokeze, ee unayeomba
maovu uwache.’

“Malaika huyo anaendelea kutangaza mpaka asubuhi, na siku inapokucha, yeye huondoka kurejea kwenye miliki ya mbinguni. Hii ndio tafsiri sahihi iliyopokelewa kutoka kwa mababu zangu ambao walisimulia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)’”5

Kupaa Kwa Mtukufu Mtume (S.A.W.W.)

Yunus bin Abd ar-Rahman anasema kwamba yeye alimuuliza Imam Musa bin Ja’far al-Kadhim (a.s.):

“Kwa nini Mwenyezi Mungu alimnyanyua Mtume Wake Mtukufu (s.a.w.w.) hadi mbinguni, na kutoka hapo hadi kwenye kituo cha mbali, Sidratul Muntaha, na halafu kwenye mapazia ya nuru, wakati alipomhutubia na kuongea naye, ambapo Mwenyezi Mungu haelezewi kwa namna ya kuwa na makazi au mahali?”

Imam (a.s.) akamjibu:

“Kwa kweli, hakuna mahali au sehemu inayohusishwa kwa Mwenyezi Mungu, wala Yeye hatawaliwi na wakati! Yeye alimnnyanyua Mtume Wake (s.a.w.w.) kuwapa heshima Malaika na wale wanaoishi katika mbingu na kuwatukuza kwa kuwepo kwake miongoni mwao.

Pia kumuonyesha yeye maajabu ya uumbaji Wake mkuu ili aje kuyaelezea kwa watu hapa duniani yale

aliyoyaona. Haikuwa kabisa katika namna watu hawa wanavyohusisha sifa za kibinadamu kwa Mwenyezi Mungu! Sifa njema kwa Mwenyezi Mungu! Yeye yuko mbali kabisa na washirika wanaowahusisha Naye."6

Katika hadithi iliyosimuliwa na Abu Basiir, Imam Ja'far Sadiq (a.s.) alitoa maelezo mapana na yenye kuondoa shaka akielezea msimamo wa Madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) juu ya suala la *Tawhiid*:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu, hawezi kuelezewa kwa namna ya kuwa na makazi au mahali. Hakuna mwendo, uzito, kubadili mahali, kuhamia au uhamisho unaovumishwa juu Yake, kwa sababu Yeye ndiye Muumba wa wakati, nafasi, mwendo, uzito. Yeye ameepukana, na yuko mbali sana na yale wanayoyasema kumhusu Yeye.7

Imam Zainul Abidiin (a.s.), katika jibu la kinaganaga kwa mwanawe Zaid, ametoa maana halisi ya Ayah fulani ambazo, kama zikitafsiriwa neno kwa neno, zitathibitisha kuwepo kwa kituo au makazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hebu tuzichunguze Ayah hizo:

عَلَىٰ أَثَرِي وَعَجِلْتُ إِلَيْكَ رَبِّ لِتَرْضَىٰ {84}

"...Na nimeharakia kwako, Mola Wangu, ili uweze kuridhia." **(*Twaha; 20: 84*)**

فَفِرُّوا إِلَى اللَّهِ ۚ {50}

"Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu ..." **(*Dhariyaat; 51: 50*)**

Imam (a.s.) akasema:

"Ayah hizi haziashirii mahali popote ambapo Musa alikwenda kukutana na Mola Wake, au ambako sisi tunaamriwa kukimbilia. Hizi ni tamathali za semi, ambazo zinamaan- isha kuziendea radhi za Mwenyezi Mungu na mwongozo Wake."

Halafu akatoa mifano ifuatayo:

تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ {4}

"Malaika na roho hupanda kwenda Kwake ..." **(*Maa'rij; 70: 4*)**

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ ۚ {10}

"...na Kwake hupanda maneno mazuri, Naye hukipandisha kitendo kizuri. (***Faatir; 35: 10***)

"Katika mifano yote miwili ya hapo juu, Mwenyezi Mungu anazungumzia vituo maalum vilivyoonyanyuliwa katika milki ya kimbinguni. Kuvifikia vituo hivyo vilivyoonyanyuliwa ni sawa na kujitahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu."8

Ndani ya Qur'ani Tukufu, imo mifano mingi ya ujenzi milikishi ambamo ndani yake ile nomino inayopingwa imeachwa. Katika *al–Burhan fi Uluum al–Qur'an,* Zarkash anasema:

"Wanasema kwamba imo takriban mifano elfu moja ndani ya Qur'ani Tukufu ambamo ile nomino iliyoambatishwa imeachwa kutoka kwenye ujenzi milikishi. Na hili limekuwa limekubalika kama tamathali ya semi ya kawaida ya wanazuoni."

Kama mfano, tutaichunguza Ayah ifuatayo:

وَاسْأَلِ الْقَرْيَةَ الَّتِي كُنَّا فِيهَا {82}

"Na waulize (***watu wa***) ***mji tulimokuwemo..."*** (***Yusuf; 12: 82***)

Neno lililoachwa ni Ahl – likiwa na maana ya "watu." Kile haswa anachotaka kukifikisha Mwenyezi Mungu ni: **"Na waulize (watu) wa mji..."**

Lakini uachwaji huu umedokezwa, na msomaji yoyote mwenye busara ataweza mara moja kuuelewa udokezwaji wake. Kwa kuegemea kwenye namna hii ya uzungumzaji, Imam ar–Ridha (a.s.) aliielezea Ayah ifuatayo: **"Na Mola Wako atakuja ..."** Nomino iliyofichwa au neno lililodokezwa hapa ni *Amr*, ambalo linamaanisha "hukumu" au "agizo", na kwa hiyo Ayah ina maana: **"Na (amri ya)Mola wako itakuja....."**

Kwa uwazi kabisa Imam (a.s.) aliegemeza ufafanuzi wake juu ya Ayah zifuatazo kutoka kwenye Qur'ani Tukufu ambamo neno Amr limetajwa pamoja na "kuja kwa Mola."

يَا إِبْرَاهِيمُ أَعْرِضْ عَنْ هَٰذَا ۖ إِنَّهُ قَدْ جَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ ۖ وَإِنَّهُمْ آتِيهِمْ عَذَابٌ غَيْرُ مَرْدُودٍ {76}

"Ewe Ibrahim! Usiyafuate haya kwa sababu amri ya Mola wako imekwishafika na hakika hao

itawafikia adhabu isiyorudishwa.” (***Huud; 11: 76***)

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَٰكِنْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ ۖ فَمَا أَغْنَتْ عَنْهُمْ آلِهَتُهُمُ الَّتِي يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ لَمَّا جَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ ۖ وَمَا زَادُوهُمْ غَيْرَ تَتْبِيبٍ {101}

“Nasi hatukuwadhulumu, bali wao wamejidhulumu wenyewe, na waungu wao waliokuwa wakiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu hawakuwafaa kitu ilipokuja amri ya Mola wako, na hawakuwazidishia ila maangamizo.” (***Huud;11:101***)

Katika Ayah zote hizo hapo juu, kile kitenzi, **“ilipokuja”** kimeandamana na uundaji milikishi “ *Amru Rabbika*, amri ya Mola Wako”. Hii inawasilisha ile maana iliyokusudiwa ya **“kuja kwa Mola wako”,** hapa duniani au katika Siku ya Hesabu.

Madhehebu ya Makhalifa ilipendekeza kigoda au kiti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na baadaye wakabuni pazia au kizuizi ambacho nyuma yake ndipo Yeye anapoishi!! Hili na mengine mengi yataunda maudhui ya mazungumzo yetu yanayofuata.

---

1. Sahih Muslim – uk. 522.
2. Sahih Muslim – uk. 522
3. ar–Radd ala al–Jahmiyyah, cha Darami – uk. 24, 26 na 27..
4. Tawhiid cha Saduuq – uk. 162.
5. Tawhiid cha Saduuq – uk. 176.
6. Tawhiid cha Saduuq – uk. 175
7. Tawhiid, cha Saduuq – uk. 183–184
8. Tawhiid, cha Saduuq

Sura Ya Nane: Mwenyezi Mungu Nyuma Ya Pazia

Darami, katika kuwakanusha kwake hao Jahmiyyah, anao mlango mzima unaoitwa *Al–Ihtijaj*, na yeye ananukuu hadith tatu zifuatazo ambazo zimehusishwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

(i) Jabir Ansari anasema:

“Mtume (s.a.w.w.) amesema kwamba Mwenyezi Mungu hakuzungumza na yeyote kamwe isipokuwa

kutoka nyuma ya pazia.”

Ni dhahiri kabisa, hadithi hii inahusiana na Ayah ifuatayo:

وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُكَلِّمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ {51}

“Na haikuwa kwa mtu yeyote kwamba Mwenyezi Mungu aseme naye ila kwa wahyi au kwa nyuma ya pazia .....” (***As-Shuraa; 42: 51***)

Wameipokea ile maana halisi ya neno pazia – kipande cha nguo, pazia linalomficha Mwenyezi Mungu kutoka kwa watu; na wameendelea kubuni vipande vingi vya kuvutia vya kipuuzi.

Hapa kuna hadithi nyingine:

(**ii**) Abu Musa Ashari anasimulia kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.):

“Pazia la Mwenyezi Mungu ni ‘Moto!’”

(**iii**) Zurarah bin Awfa anasimulia:

“Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimuuliza Jibril kama alikuwa amewahi kumuona Mola Wake. Jibril akajibu: Oh, Muhammad! Kati Yake na mimi kuna mapazia sabini ya nuru; na kama nitajaribu kusogea karibu na hilo la kwanza, basi nitaungua.’”

Licha ya hizi hadithi tatu, ipo moja ya nyongeza kutoka kwa Abdullah bin Umar, ambaye amesema:

“Mwenyezi Mungu amefichikana kwa waja Wake kwa mapazia ya Moto, Giza na Mwanga.”

Mwishoni, Darami anamalizia kwamba:

“Ile hadithi ya Jibril inaashiria wazi kwamba Mwenyezi Mungu yuko nyuma ya pazia, na kwa hiyo amejitenganisha na viumbe Wake. Kwa hiyo, kama ingekuwa kweli kwamba ni Mwenye kupatikana kila mahala, basi kuwepo kwa pazia kungekuwa hakuna maana yoyote.”

Wanazuoni kutoka Madhehebu ya Makhalifa wametegemea sana juu ya maana halisi ya neno Hijab, ambalo linatokea kwenye Ayah kadhaa za Qur’ani Tukufu.

Kwa mfano, katika hiyo Ayah iliyonukuliwa hapo juu kutoka kwenye Surah ya As-Shuraa: 51, kifungu cha maneno, “kutoka nyuma ya pazia” ni cha kiistiari kinachodokeza kwamba Mwenyezi Mungu anazungumza na watu katika namna kwamba sauti inasikika bila ya mzungumzaji kuonekana.

Hakuna pazia la kimaada hapo la kumtenganisha Mwenyezi Mungu na hao Mitume, kwani kwa hali hiyo,

Mwenyezi Mungu atakuwa amezuilika mahali – wazo ambalo ni geni kabisa kwenye dhana ya asili ya Mwenyezi Mungu katika Uislamu.

Ayah nyingine ni hii:

كَلَّا إِنَّهُمْ عَنْ رَبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَمَحْجُوبُونَ {15}

"Sivyo, hakika kwa Mola wao, siku hiyo watakingiwa na pazia." **(*Mutaffifiin; 83: 15*)**

Imam Fakhruddin ar-Razi ndani ya *Tafsiir* yake (31/96, chapa ya Misri) anasema:

"Ni muhimu kwamba tunaitafsiri Ayah hii kumaanisha kwamba wale makafiri watazuiliwa kumuona Mwenyezi Mungu, kwa njia ya kuwekewa pazia."

Kisha anatafuta uthibitisho kutoka kwa Maqatil ambaye amesema:

"Hilo pazia linaelezea kwamba baada ya kufufuliwa na kuhesabiwa, wale makafiri hawatamuona Mwenyezi Mungu. Kwa kweli wale waumini watamuona Yeye."

Imam wa madhehebu ya Maliki, yaani Malik bin Anas anasema: "Kwa vile Mwenyezi Mungu atakuwa nyuma ya pazia, akiwa amefichika kutoka kwa maadui Zake, atadhihirisha utukufu wake juu ya marafiki Zake ili waweze kumuona Yeye."

Na Muhammad ibn Idriis, maarufu sana kwa jina la Shafii' anaielezea Ayah hiyo hivi:

"Kwa vile Mwenyezi Mungu Mwenyewe atajificha kutokana na maadui Zake ili kudhihirisha ghadhabu Zake, ni dhahiri kwamba atajidhihirisha Mwenyewe kwa wale ambao ni marafiki Zake kuonyesha radhi Zake."

Ibn Kathiir, ndani ya *Tafsiir* yake ameyatwaa yale maelezo ya Imam Shafii'! Hebu sasa tugeukie kwenye kile ambacho Ahlul-Bayt (a.s.) wamekieleza.

Je, Kuna Pazia?

(1) Saduuq ndani ya *Tawhiid* yake anasimulia hadithi fupi ya kuvutia kutoka kwa Haarith al-Aawar. Yeye anasema wakati mmoja ambapo Ali bin Abi Talib (a.s.) alipoingia eneo la sokoni, alimsikia mtu mmoja ambaye alikuwa amesimama akiwa amempa kisogo, akisema maneno yafuatayo: *"Naapa kwa Yeye Ambaye yuko nyuma ya pazia mbele ya zile mbingu saba!"* Ali bin Abi Talib alimpiga mgongoni mwake na kuuliza: "Na ni nani aliyeko mbele ya hizo mbingu saba?"

Yule mtu akasema: "Oh, Amirul Mu'minin, nilimaanisha 'Mwenyezi Mungu' alikuwa nyuma ya pazia."

Ali (a.s.) akasema:

“Hiyo kwa hakika ni dhambi kubwa. Hakuna kifuniko au pazia linalomtenganisha Mwenyezi Mungu kutoka kwa viumbe Wake. Yeye yupo kila mahali!”

Yule mtu akamuuliza Ali bin Abi Talib (a.s.) kama kulikuwa na kitendo cha toba cha lazima ili kufidia ile dhambi aliyoifanya.

Ali (a.s.) akasema:

“Fidia yake ni kuelewa vizuri na kwa dhahiri kwamba Yeye yuko pamoja na wewe mahali popote utakapokuwa.!” Yule mtu akauliza tena: “Je, ninapaswa kulisha masikini kama fidia ya hilo?” Ali (a.s.) akasema: “Hilo pia haliingii hapa, kwa sababu umeapia kwa jina la mmoja ambaye siye Mola wako.”

Maoni

(i) Katika hadithi fupi ya hapo juu, tunaona mtu amekula kiapo, ambacho ni cha uasi. Imam Ali (a.s.) anamwelekeza yeye kufidia kule kupotoka kwa kuielewa Tawhiid katika muundo wake halisi. Anamuathiri kwa ule ukweli kwamba hakuna mapazia wala maficho na kwamba Mwenyezi Mungu Yupo mahali pote.

(ii) Wakati mtu huyo huyo akiuliza kama anapaswa kufidia kwa ajili ya kiapo alichokichukua, Imam (a.s.) anarudia kusema kwa kumwambia kwamba lengo la kiapo chake halikuwa ni Mwenyezi Mungu – na kwa hiyo kiapo hicho hakikuwa na thamani yoyote ile iwayo.

(2) Saduuq katika *Tawhiid* yake anasimulia kwamba Imam Ridha (a.s) aliombwa kuelezea juu ya Ayah ifuatayo:

كَلَّا إِنَّهُمْ عَنْ رَبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَمَحْجُوبُونَ {15}

“Sivyo, hakika kwa Mola wao, siku hiyo watakingiwa na pazia.” **(*Mutaffifiin; 83: 15*)**

Akasema

“Hakuna mahali mahsusi panapoweza kuhusishwa maalum kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa maana ya kwamba anakaa hapo, na kutokea hapo anachukua pazia kujitenga Mwenyewe kutoka kwa viumbe Wake. Maana halisi ya Ayah hiyo ni kwamba: ‘…wao watazikosa rehema za Mola Wao.’”

Halafu aliulizwa kuhusu Ayah ifuatayo:

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَهُمُ اللَّهُ فِي ظُلَلٍ مِنَ الْغَمَامِ وَالْمَلَائِكَةُ {210}

"Hawangojei ila Mwenyezi Mungu awafikie katika vivuli vya mawingu na Malaika." **(*al-Baqarah; 2:210*)**

Imam (a.s.) akasema:

"Hii haipaswi kufasiriwa kwa maana ya neno kwa neno. Kile kitu ambacho kitatoka humo kwenye mawingu meusi, kitakuwa ni Amri Yake, Adhabu Yake. Ni istiari ambamo ile nomino pinzani imeachwa katika huo uundaji milikishi (*genitive construction*)."

Mtu anajaribu kufikiri kwamba wanazuoni kutoka kwenye madhehebu ya upande wa pili, baada ya kuwa wamejitenga wao wenyewe kutoka kwa Ahul-Bayt (a.s.) wameangukia kuwa mateka wa utomaji maneno wa Kiyahudi na Kikristo, pamoja na kutojali kabisa kile ambacho Qur'ani Tukufu yenyewe inachofundisha.

Katika *Suratun-Nisa*, Ayah ya 108, Allah swt. anasema:

يَسْتَخْفُونَ مِنَ النَّاسِ وَلَا يَسْتَخْفُونَ مِنَ اللَّهِ وَهُوَ مَعَهُمْ إِذْ يُبَيِّتُونَ مَا لَا يَرْضَىٰ مِنَ الْقَوْلِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ بِمَا

يَعْمَلُونَ مُحِيطًا {108}

"Wanajificha kwa watu wala hawamstahi Mwenyezi Mungu, naye yu pamoja nao pale wanaposhauriana usiku kwa maneno asiyoyapenda na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua vyema yale wayatendayo." **(*An-Nisaa; 4:108*)**

Kuna Ayah nyingine iliyopo katika *Sural-Mujadilah*, Ayah ya 7, ambayo inasema:

"Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini? Hawashauriani kwa siri watatu ila yeye ni wa nne wao, wala watano ila yeye ni wa sita wao, wala wachache kuliko hao wala zaidi ila yeye huwa pamoja nao popote walipo. Kisha Siku ya Kiyama atawaambia yale waliyoyatenda, hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."

Hivyo liko wapi pazia hapo? Liko wapi wazo la kujitenga na viumbe vyake? Ilikuwa ni dhana hii, ambamo mwisho wake uliwafanya wao kuamini kwamba wale waumini watamuona Mwenyezi Mungu waziwazi hiyo Siku ya Kiyama.

Sura Ya Tisa: Kuona Kwa Mwenyezi Mungu

Madhehebu ya Makhalifa wamezungumzia kuona kwa Mwenyezi Mungu katika namna tatu.
Nazo hizo ni:

(i) Mwenyezi Mungu anaona kupitia kwa Mtume wetu (s.a.w.w.) wakati wa uhai wake;

(ii) Mwenyezi Mungu anaona kupitia kwa waumini katika hiyo Siku ya Kiyama, kabla hawajaingia Peponi;

(iii) Mwenyezi Mungu anaona kupitia kwa waumini wakati wa kukaa kwao ndani ya Pepo.

Ibn Khuzaimah ndani ya *Tawhiid* yake anasimulia kutoka kwa Ibn Abbas, Abu Dharr na Anas hadithi inayounga mkono imani ya kwamba Mtume wetu (s.a.w.w.) alimuona Mwenyezi Mungu.

Kwa mfano, kutoka kwa Ibn Abbas yeye anasimulia kwamba Mwenyezi Mungu alimbariki Nabii Ibrahim (a.s.) kwa kumchukulia yeye kama rafiki, Nabii Musa (a.s.) kwa kuzungumza naye, na Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kwa kujionyesha Yeye Mwenyewe kwake. Katika nyingi ya hadithi kama hizi, Ikramah, yule mtumwa aliyeachwa huru na Ibn Abbas ametajwa. Ikramah anafahamika sana kwa kuhusisha hadithi za uongo kwa Ibn Abbas.

Kwa upande mwingine tunajua kwamba Ibn Abbas alikuwa miongoni mwa masahaba na wanafunzi wa karibu sana wa Imam Ali ibn Abi Talib (a.s.). Ni jambo lisilowazika kwamba Ibn Abbas angeweza kueleza jambo lolote, ambalo linakwenda kinyume na mafundisho ya Ahlul-Bayt (a.s.). Ukweli ni kwamba Ibn Khuzaimah alikuwa chini ya ushawishi wa Ka'b al-Ahbar ambaye ndiye anayemnukuu:

"Mwenyezi Mungu amezigawanya neema Zake mbili maalum kati ya Musa na Muhammad – zawadi ya mawasiliano ya moja kwa moja na zawa- di ya kumuona Mwenyezi Mungu. Hivyo Muhammad (s.a.w.w.) alimuona Yeye mara mbili, na Musa aliongea Naye mara mbili."1

Ni lazima ielezwa kwamba wanazuoni fulani na masahaba walio kinyume na Madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) wamekataa kwa ushupavu kabisa kuamini kwamba Mtume wetu (s.a.w.w.) aliwahi kumuona Mwenyezi Mungu kamwe. Miongoni mwao ni Bi. Aisha, mkewe Mtume mwenyewe. Lakini Ibn Khuzaimah anasisitiza juu ya ukweli wa ile hadithi kutoka kwa Ka'b al-Ahbar na kumkanusha Aisha.

Katika hadithi ndefu ifuatayo kutoka kwa Abu Huraira, inayosimuliwa na Bukhari, Muslim, Abu Dawuud, Ibn Majah, Tirmidhi, Ahmad bin Hanbal na Suyuti, tunakutana na tamthiliya ambayo inadhaniwa kuja kujidhihirisha yenyewe mnamo Siku ya Kiyama. Abu Huraira anasema:

"Baadhi ya watu waliuliza: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je, tutakuja kumuona Mola wetu hiyo Siku ya Kiyama?' Mtukufu Mtume akajibu:

'Je, mnatilia shaka juu ya kuliona jua katika siku angavu?' Wao wakasema: 'Laa hasha, Ewe Mtume.'

Mtume Mtukufu akasema: ‘Hivyo mtamuona Yeye mnamo Siku ya Kiyama! Mwenyezi Mungu atawakusanya watu wote na halafu atatangaza: Kila mmoja amfuate mungu wake aliyekuwa akimuabudu. Baadhi yao watalifuata jua, na wengine mwezi. Wachache wao watakwenda nyuma ya mashetani. Kisha watu wa Umma, pamoja na wanafiki watabakia imara. Halafu Mwenyezi Mungu atajionyesha Mwenyewe, pamoja na sura ambayo itakuwa ngeni kwao, na atasema: Mimi hapa, Mola Wenu!’

“Wataguta kwa sauti kubwa: ‘Tunaomba hifadhi kwa Mola Wetu kutokana na wewe. Sisi tutakaa hapa hadi Mola Wetu atakapokuja. Na hapo atakapokuja, sisi tutamtambua Yeye.’

“Halafu Mwenyezi Mungu atatokeza kwa ule uso unaofahamika na kusema: ‘Mola Wenu Mimi hapa!’

“Wao watasema: ‘Ndiyo, Wewe hakika ndiye Mola Wetu.’ Halafu watamfuata Yeye na Mwenyezi Mungu atairudisha mahali pake ile daraja juu ya Moto wa Jahannam.”
Halafu Abu Huraira anaendelea zaidi kutoa maelezo kuhusu moto wa jahannam, na kuelezea jinsi ambavyo hatimaye waumini watakavyokuja kuokolewa kutokana na adhabu. Kisha akasema:

“Mtu mmoja atakuja kuachwa nyuma na uso wake ukiwa umeelekea moto ulioghadhibika. Atasema: ‘Ewe Mola Wangu! Ile harufu mbaya ya moto wa jahannam imenisumu, na miale yake imenibabua. Nigeuze uso wangu mbali kutoka kwenye moto wa jahannam.’

“Atarudia kusihi kwake mara nyingi, mpaka Mwenyezi Mungu atakapose– ma: ‘Kama nitakukidhia haja yako, utaomba mengi zaidi.’ Mtu huyo atasema: ‘Kwa Utukufu Wako, mimi sitaomba tena zaidi ya hayo.’

“Mwenyezi Mungu ataugeuzia mbali uso wake kutoka kwenye moto wa jahannam. Papo hapo, mtu huyo atasema: ‘Ewe Mola Wangu, nipeleke karibu na milango ya Peponi.’

“Mwenyezi Mungu atasema: ‘Je, wewe hukuahidi kwamba hutakuja kuomba kitu chochote kile kingine? Ole wako, ewe mwana wa Adam! Wewe ni mdanganyifu.’

“Lakini mtu huyo atasisitiza. Hivyo Mwenyezi Mungu atakuja kusema: “Je, utakuja kuomba kitu kingine tena kama nitakukubalia hilo?’

“Mtu huyo atakujasema: ‘Hapana, kwa Utukufu Wako, Mimi sitakuja kuomba tena.’

“Na atakuja kutoa ahadi ya dhati; na Mwenyezi Mungu atamchukua yeye hadi kwenye milango ya Peponi. Pale yeye atakapoziona rehema zilizosheheni ndani ya Pepo, atanyamaza kimya na kusimama kwa heshima na mshangao kwa kitambo kiasi, na halafu atasihi: Oh, Mola Wangu, niruhusu kuingia Peponi.’

“Mwenyezi Mungu atasema: ‘Wewe hukuahidi kutoomba chochote zaidi? Ole wako ewe mwana wa Adam! Kwa hakika wewe ni mdanganyifu.’ Lakini mtu huyo ataendelea kuomba kwa kung’ang’ania na kusihi mpaka Mwenyezi Mungu atacheka – na kicheko hicho kitaashiria ruksa.

Wakati mtu huyo hatimaye atakapokanyaga ndani ya Pepo, atapewa haja zake zote, hadi iwe hakuna cha kuhitaji tena.

Halafu Mwenyezi Mungu atasema: 'Yote haya, na maradufu zaidi, ni kwa ajili yako.'"

Abu Hurair akaongeza: "Mtu huyo atakuwa mtu wa mwisho kuingia Peponi."

Huu ni mfano kutoka kwenye vyanzo sahihi vya madhehebu ya Makhalifa. Sasa hebu tuchunguze ni nini Ahlul-Bayt (a.s.) walichosema:

Mwenyezi Mungu Hawezi Kuonekana

Maimam wa Ahlul-Bayt (a.s.) wamefundisha kwa uthabiti kabisa kwamba suala la kudhihiri na kuonekana halitumiki kwa Mwenyezi Mungu. Yeye hataonekana hiyo Siku ya Kiyama, na hawezi kuonekana hapa juu ya ardhi vilevile.

(1) Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.) amesema:

"Mmoja wa watu wasomi kutoka kwa watu wa vitabu alikwenda kwa Imam Ali (a.s.) na akamuuliza: 'Ewe Ali, je, umewahi kumuona Mola Wako kamwe wakati wa kufanya kwako ibada?'

Imam Ali (a.s.) akasema: 'Mimi sijamuabudu kamwe Yule ambaye sija muona!'

Yule mwanazuoni akauliza: 'Na ulimuona vipi Yeye?'

Imam (a.s.) akasema: 'Kumbuka, hili jicho la kimwili haliwezi kumuona Yeye.
Ni moyo ndio ambao unamuona Yeye pamoja na imani halisi'"2

(2) Safwan bin Yahya anasema kwamba Abu Qurrah, mmoja wa wapokezi wa madhehebu ya Makhalifa, aliomba ruhusa ya kuonana na Imam ar- Ridhaa (a.s.). Baada ya kuruhisiwa kufika mbele ya Imam, aliwasilisha maswali kadhaa yaliyohusiana na Shariah ya Kiislamu (*fiqh*). Halafu akasema:

"Tunayo hadithi ambayo inasema kwamba Mwenyezi Mungu aligawanya neema Zake kati ya Nabii Musa (a.s.) na Muhammad (s.a.w.w.). Pamoja na huyu wa mwanzo, Yeye alizungumza naye, na huyu wa baadaye (s.a.w.w.), Yeye alijidhihirisha Mwenyewe kwake."

Baada ya kuyasikia haya, Imam ar-Ridhaa (a.s.) akasema:

"Kama hivyo ndivyo ilivyokuwa, basi ni nani aliyefikisha ujumbe ufuatao kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

لَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ ۖ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ {103}

(***a***) ***"Macho hayamfikii, bali Yeye anayafikia macho, naye ni Mwenye kujua, Mwenye habari."*** (***Al-An'aam; 6: 103***)

وَلَا يُحِيطُونَ بِهِ عِلْمًا {110}

(***b***) ***"...wala hawataweza kumjua*** (***Mwenyezi Mungu***) ***vilivyo kwa elimu zao."*** (***At-Twaha; 20: 110***)

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ {11}

(***c***) ***"Hakuna chochote mfano wake, naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona."*** (***As-Shuraa; 42: 11***)

"Je, haikuwa ni Muhammad (s.a.w.w.) aliyefikisha ujumbe huu mtukufu?"

Abu Qurrah akasema: "Ndiyo, hakika, alikuwa ni Muhammad (s.a.w.) ambaye alifikisha."

Imam ar-Ridha (a.s.) akasema:

"Inawezekana vipi mtu aliyewafundisha wanadamu kwamba Mwenyezi Mungu hawezi kuonekana, kuzingirwa, kufananishwa au kulinganishwa, ghafla ageuke na kusema: 'Mimi nimemuona Yeye, nikamzingatia, na kwamba anafanana na mwanadamu?' Huoni aibu au haya kumzulia Mtume (s.a.w.w.) mambo ambayo hata wale wasioamini hawakumhusisha nayo?"

Abu Qurrah akasema:

"Lakini Qur'ani Tukufu inasema kwamba katika usiku wa Mi'raaj Mtume alimuona Mwenyezi Mungu."

Halafu akasoma Ayah ifuatayo:

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ {13}

"Na bila shaka yeye alikiona kwa mara nyingine"(***An-Najmi; 53: 13***)

(Abu Qurrah alishikilia kwamba kile kitenzi **"hu"** – katika ***ra'ahu*** – kina- paswa kumaanisha **"Yeye,"** yaani Mwenyezi Mungu).

Imam ar-Ridha (a.s.) akasema:

"Ni lazima uisome ile Ayah inayofuatia ambayo inaelezea kile Mtume (s.a.w.w.) alichokiona. Katika Ayah

ya 18 ya Surah hiyo hiyo, unakuta:

لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ {18}

“Kwa hakika aliona katika dalili za Mola wake zilizo kuu.” **(*An-Najmi; 53: 18*)**

“Dalili za Mwenyezi Mungu sio Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hawezi kuonekena – hakuna macho yanayoweza kumzingatia Yeye na hakuna elimu inayoweza kumzingira.”

Abu Qurrah akalalamika: “Kwa hiyo unazichukulia hadithi zetu kama uongo?”

Imam ar-Ridha (a.s.) akasema: “Hadithi yoyote ambayo inakwenda kinyume na Qur’ani Tukufu ni uongo, na imehusishwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa uongo. Siitolei usadik- isho juu yake.” 3

Yenye Kuonekana Wazi Katika Hadithi Kutoka Kwa Abu Huraira

1. Kwamba Mwenyezi Mungu ataonekana katika Siku ya Kiyama, kwa kung’ara na dhahiri kabisa kama jua au mwezi katika anga nyeupe;

2. Kwamba Mwenyezi Mungu atatokeza kwanza kwa uso usiofahamika, kwa matokeo kwamba Waislamu hawataweza kumtambua. Yeye atatokeza tena na sura inayofahamika na halafu atakubalika kwa waumini;

3. Kwamba mtu aliyeuelekea moto wa jahannam ataendelea kumdan- ganya Mwenyezi Mungu mara tatu;

4. Kwamba Mwenyezi Mungu atakuja kucheka, kwa namna sisi binadamu tunavyocheka.

Abu Huraira anaonekana kuelekea kumwelezea Mwenyezi Mungu kama chalii mchezi anayebadili sura yake kufurahisha watu.

Mtu anashangaa ni sifa gani maalum za sura Yake ambazo Waislamu watazitambua? Je, wao wamewahi kumuona kabla ya hapo? Kama ndivyo, ilikuwa lini? Ilikuwa wakati Alipokuwa Kijana, Mzee, au alipokuwa kapondwa kabisa na umri mkubwa ?

Hata lile Agano la Kale au Jipya yote hayana kisa cha ajabu kama hicho. Ni hekaya za bibi kizee zinazosimuliwa kwa mtoto wakati wa usiku mrefu wa baridi kali! Lakini athari za utungaji maneno ya uongo huu umekuwa mkubwa mno. Mawahabi na wanazuoni wengi wengine kutoka madhehebu ya Makhalifa wanashikilia kwamba Mwenyezi Mungu atakuja kuonekana kimwili, wazi wazi katika Siku ya Kiyama.

Mikazo Ya Wazi Ya Ufafanuzi Wa Ahlul-Bayt (A.S.)

(a) Kwamba macho yanaweza kufahamu tu vile vitu, ambavyo vina mwili au maada;

(b) Chochote kilichopo ambacho hakina mwili, (kwa mfano roho, mwanga, umeme n.k.) hakiwezi kuonekana. Kwa kweli suala la kukiona kiumbe kama hicho halina msingi, halipasiki;

(c) Mwenyezi Mungu sio mwili wala maada. Yeye ndiye Muumba wa maada. Mtu anaweza 'kumuona' Yeye kupitia kwenye viumbe Vyake;

(d) Hakuna chochote kile kiwacho chenye kufanana Naye, hivyo Yeye hawezi kulinganishwa na umbile lolote lile;

(e) Hadithi yoyote ile, ambayo inakwenda kinyume na Qur'ani Tukufu, ni lazima itupiliwe mbali kama ya uongo.

---

1. Tawhiid, cha Ibn Khuzaimah – uk.202
2. Tawhiid, cha Saduuq – uk.109.
3. Tawhiid cha Saduuq – uk. 110 – 112.

Sura Ya Kumi: Kukutana Na Mwenyezi Mungu

Kuwa Pamoja Na Mwenyezi Mungu Ndani Ya Pepo

Licha ya hayo yaliyokwisha kutangulia, inasikitisha na kuvutia kuona kwamba Madhehebu ya Makhalifa imeruhusu fikra zao kwenda zitakavyo kuhusiana na kukutana na Mwenyezi Mungu katika masoko ya Peponi!

(1) Ibn Majah na Tirmidhi wamesimulia mazungumzo yafuatayo ndani ya Sunan zao. Abu Huraira wakati mmoja alimwambia Sa'id bin al-Musayyab:

"Mimi ninaomba kwamba tuweze kukutana pamoja katika soko la Peponi!"
Sa'id akamuuliza: "Hivi kuna soko ndani ya Pepo?"

Abu Huraira akasema: "Ndio hivyo, lipo! Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alinifahamisha mimi kwamba wakati watu wa Peponi watakapoingia humo, watawekwa kulin- gana na daraja za ubora katika matendo yao. Halafu wataruhusiwa kumtembelea Mwenyezi Mungu kwa kipindi cha wakati sawa na siku ya Ijumaa

duniani. Hivyo watamtembelea Yeye, na atawaonyesha Kiti Chake cha Enzi, na kujidhihirisha Mwenyewe katika moja ya mabustani ya Peponi.

Kisha atawawekea majukwaa au mimbari za nuru, lulu, johari, kito mchanganyiko wa chuma/manganizi – ***chrysolite***, na dhahabu. Mtu wa chini sana miongoni mwao atakuwa amewekwa kwenye malundo ya maski na kafuri, bila kujihisi kabisa kwamba wale watu walioko kwenye mimbari wamewekwa pazuri zaidi!"

Abu Huraira akaendelea :

"Halafu nikamuuliza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je, tutamuona Mola Wetu?" Yeye Mtume akasema: 'Je, mna mashaka ya kuliona jua au mwezi kamili?' Sisi tukasema: 'La hasha, hatuna mashaka.' Yeye akasema: 'Kwa hiyo bila shaka mtamuona Mola Wenu Mtukufu. Kila mmoja wenu atain- gizwa kwenye hadhara Yake peke yake, na halafu kwa mmoja wenu Yeye Atakuja kumwambia: Ewe fulani bin fulani! Je, unaikumbuka ile siku ulipotenda tendo kadha na kadhaa?' Yeye atajibu: 'Ewe Mola Wangu! Hivi ulikuwa hukunisamehe!?

"Mwenyezi Mungu atasema: 'Kwa kweli Nilikusamehe. Ni upana wa huruma Yangu ambao umekuleta wewe hapa kwenye kituo hiki!" Halafu wingu kutoka juu litawafunika, na itakuwepo mvua ya mfululizo ya manukato, ambayo harufu yake wao watakuwa hawajapata kuinusa kamwe. Mwenyezi Mungu Atasema: 'Amkeni mfurahie neema Zangu na chukueni kila mtakachokitaka.'

Kisha tutafika kwenye soko tukiungana na Malaika. Ndani yake mtakuwa na vitu ambavyo mfano wake hatujawahi kuuona au kusikia au kudhania. Tutachukua chochote tunachotaka – hakuna kununua, wala hakuna kuuza! Watu watatembeleana, wale wa juu wakikutana na wa chini, na kwa hakika hakutakuwa na uduni, kwani kila mmoja atakuwa amevishwa vizuri, na katika welekeo bora. Hakutakuwepo na kitu cha kuhuzunikia.

Halafu tutarudi kwenye sehemu zetu, ambako wake zetu wenyewe watatupokea. Wao watasema: "Karibuni, mmerudi mkiwa watanashati zaidi na wazuri zaidi kuliko mlivyokuwa wakati ule mlipotuacha!" Sisi tutasema: "Tunastahiki kurudi na neema hizi kwa sababu leo tumekaa na Mola Wetu."

Asili ya simulizi hii ya uongo inaweza kupatikana katika hadithi ifuatayo kutoka kwa Ka'b al-Ahbar, iliyosimuliwa na Darami katika kitabu chake akiikanusha madhehebu ya Jahmiyyah. Ka'b anasema:

"Mwenyezi Mungu hataikagua Pepo isipokuwa kusema:

'Kuweni harufu nzuri kwa wenza wenu.' Kisha patakuwepo na ongezeko la harufu nzuri mahali pote hapo. Na kwa muda wa kitambo sawa na siku ya Iddi hapa duniani, watatembea huko na huko katika mabustani ya Peponi. Mwenyezi Mungu ndipo atakapotokeza, na wao watamuona Yeye. Upepo mkali uliojaa harufu ya manukato na miski utavuma, na Mola Wao atawatimizia matakwa yao.

Halafu wao watarejea kwenye familia zao, ambako uzuri na utanashati wao utakuwa umeongeka mara

sabini.”1

Abu Huraira alijaribu kuufanya uwongo huu kuwa wakupendeza zaidi kwa kutumia akili yake binafsi yenye mawazo mengi. Mbali na hadithi kama hizo, tunaona kwamba wanazuoni kutoka madhehebu ya Makhalifa wamechukua uhuru mwingi katika kuzielezea Ayah fulani za Qur’ani Tukufu katika namna ya kukidhi matamanio yao.

(**2**) Qur’ani Tukufu inasema:

لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۖ وَلَا يَرْهَقُ وُجُوهَهُمْ قَتَرٌ وَلَا ذِلَّةٌ ۚ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ {26}

“Wale wanaofanya wema watapata wema na zaidi, na vumbi hal- itawafunika nyuso zao wala udhalili, hao ndio watu wa Peponi, humo wao watakaa milele.” (***Yunus; 10: 26***)

Katika Ayah hii, kile kifungu cha maneno **“na zaidi”** kilichotajwa baada ya malipo ya wema, kimechukuliwa kumaanisha upendeleo wa kukutana kwa maumbile, wazi wazi, na Mwenyezi Mungu! Tabari anasimulia kutoka kwa masahaba wanne wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambapo Suyuti anafanikiwa kusimulia kutoka kwa masahaba tisa, kwamba Mtume (s.a.w.w.) amesema:

“Ile ‘zaidi’ iliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu katika Ayah hii ina maana kwamba Mwenyezi Mungu atajionyesha Mwenyewe kwao.”2

Zaidi ya hayo, Abu Musa Ash’ari anasimulia yafuatayo kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

“Siku ya Kiyama, Mwenyezi Mungu atatuma mpiga mbiu kwa watu wa Peponi, akitangaza kwa sauti kubwa kiasi cha kutosha kuyafikia masikio ya wakazi wote akisema: ‘Mwenyezi Mungu amewaahidi wema na zaidi …’ Wema huo ni Pepo ambayo tayari mmeikalia – na hiyo zaidi ni kuu- tazama uso mtukufu wa yule Mwenye huruma.”

Tayalasi, Ahmad Hanbal, Muslim, Tirmidhi, Ibn Majah, Tabari, Suyuti na wafasiri wengine na wasimulizi wa hadithi wamesimulia yafuatayo kutoka kwa Shu’ayb:

“Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliisoma ile Ayah isemayo: **‘Wale wanaofanya wema watapata wema na zaidi …’** na kisha akasema:

“Wakati watu wa Peponi watakapokuwa wamekusanyika ndani ya mabustani na pale wengine watakapokuwa wamepelekwa kwenye Jahannam ya milele, mpiga mbiu atatangaza: ‘Enyi watu wa Peponi, bado kuna ahadi ambayo haijatimizwa ambayo Mwenyezi Mungu sasa ataitimiza!’

“Hao watu wa Peponi watauliza: ‘Na ni ahadi gani hiyo iliyobakia? Kwani hajatuweka sisi mbali na moto

wa jahannam?'

“Baada ya kuyasikia haya, Mwenyezi Mungu atanyanyua pazia, na tazama! Hapo wao watamuona Yeye. Wallahi! Katika neema zote zilizotolewa na Mwenyezi Mungu, hakuna kingine chenye kufurahisha zaidi na chenye nderemo kuliko ile fursa ya kuuona Uso Wake.”3

Ibn Kathiir katika tafsiri yake ya Ayah hiyo hiyo yeye anasema:

“Licha ya malipo mema wanayopewa wale watu wema, pia watakuwa na neema ya kuuona uso Wake Mtukkufu. Na hili limeungwa mkono na Abu Bakr Sidiq na wengineo...”

Hapa anatoa orodha ya watu kumi na tano, ambao miongoni mwao wengine ni masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na wengine ni wa zama za baadae kidogo. Hata Fakhrud-Din ar-Razi anaelekea kuunga mkono kwenye dhana hiyo hiyo, wakati anapoielezea Ayah hii. Yeye anasema:

“Tumelifanya kuwa dhahiri kwamba maneno ya Ayah hii kwa wazi kabisa yanaashiria kwamba 'na zaidi' inarejea kwenye kumuona Mwenyezi Mungu.”4

(3) Kuna baadhi ya hadithi zilizohusishwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na Ayah ifuatayo:

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَاضِرَةٌ {22}

إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ {23}

“Nyuso siku hiyo zitang'aa. Zikingoja malipo kutoka kwa Mola wao. (***Qiyaama; 75: 22-23***)

Anas bin Malik anasimulia kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.):

“Katika ufufuo, waumini wanaume watamuona Mwenyezi Mungu kila siku ya Ijumaa, na waumini wanawake watamuona Yeye katika siku za Idd-el-Fitr na Iddul-Adh'ha.”

Katika hadithi nyingine iliyosimuliwa na Anas bin Malik tunamkuta yeye akisema:

“Mtume (s.a.w.w.) aliisoma Ayah hiyo halafu akaelezea:

'Kwa jina la Allah! Ayah hii haijafutwa. Hakika wao watakuja kumuona Mwenyezi Mungu. Watapewa chakula cha kutosha ili wale na kunywa, na mgao mzuri wa manukato na mapambo. Na lile pazia baina yao na Mola wao litanyanyuliwa ili waweze kumuona Mola wao naye Mola wao awaone wao. Haya ndio aliyomaanisha Mwenyezi Mungu pale aliposema:

﴿ وَلَهُمْ رِزْقُهُمْ فِيهَا بُكْرَةً وَعَشِيًّا {62}

***'... na watapata riziki zao asubuhi na jioni'* (*Maryam; 19: 62*)**

Suyuti amesimulia yafuatayo kutoka kwa Jabir, ambaye anasema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: 'Mwenyezi Mungu ataruhusu kuonwa na hadhara ya watu wote, lakini kwa Abu Bakr kutakuwa na udhihirishaji maalum.'"5

Abdullah bin Umar anaihusisha hadithi ifuatayo kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

"Kituo cha chini kabisa ndani ya Pepo kitamruhusu muumini kupokea neema za Mwenyezi Mungu kutoka umbali wa miaka elfu moja. Na kituo cha juu kabisa kitakuwa ni pale ambapo watauona uso wa Mwenyezi Mungu kila mawio na machweo ya jua."

Tabari amerudia kusema tena imani hiyo hiyo ndani ya *Tafsiir* yake, na Fakhrudin ar-Razi ndani ya *Tafsiir Kabiir* anasema:

"Hapawezi kuwa na maana nyingine ya Ayah hii isipokuwa kule kutazama kwa wazi wazi."

Hata yule mfasiri wa hivi karibuni na mwanazuoni kutoka madhehebu ya Makhalifa, Sayyid Qutubi, (aliyefariki mwaka 1386 Hijiria) anasisitiza ndani ya kitabu chake, Fi Zilal al-Qur'an kwamba kutakuwa na kukutana uso kwa uso, kwa dhahiri na Mwenyezi Mungu katika Siku ya Kiyama, na halafu anaendelea kuitukuza hali hiyo kwa kujigamba kote. Yeye anaandika:

"Ayah hii inataja kwa kifupi juu ya hali ambayo maneno hayawezi kuelezea, na ambayo akili zinashindwa kuele- wa. Hiyo itakuwa pale watu wema watakapoingia kwenye hali ya kunyanyuliwa kiroho isiyowahi kutokea, ya kipekee, na Pepo yenyewe pamoja na neema zake na furaha itaelekea kuwa si kitu na ndogo. Hizo nyuso zinazong'ara zitakuwa zinaangalia moja kwa moja kwenye uso Mtukufu wa Mwenyezi Mungu! Kunyanyuliwa kulikoje? Ni kiwango gani cha Utukufu!

"Wakati mtu anapoangalia maajabu ya maumbile, yaliyomzunguka mwenyewe na vile vile yaliyo karibu; usiku wa mbalamwezi au giza nene, au alfajiri inayochomoza, anajawa na furaha na mzinduko! Hali yake itakuwaje, kisha, pale atakapoona, sio yale maajabu ya Mwenyezi Mungu, bali utukufu na uzuri wa Mwenyezi Mungu Mwenyewe? Kwa nini uso wake using'are kwa uangavu pale anapomuona Yeye?

"Mwanadamu hawezi kufikia hali hiyo mpaka awe amejitakasa mwenyewe kutokana na vikwazo vyote, hali adhimu sana ambayo inapaswa kutokuwa na mashaka yote na dosari – bila ya haja yoyote ila ya kumuona Mwenyezi Mungu, aliye juu, Mtukufu.

"Kwa nini watu wengine wanajinyima wenyewe hii nuru iliyozidi kabisa, hii starehe isioyoelezeka? Kwa nini wanajitatiza wenyewe katika mazoezi ya kiwanazuoni na mijadala ya hekima kuamua juu ya suala

ambalo liko nje ya akili ya kibinadamu?

“Hebu natuamke basi ili tupokee huu upeo wa muungano wa kiroho na furaha halisi na tuziruhusu fikira zetu kuizingira hii hali halisi kwa kiasi iwezekanavyo. Mzinduko huu, wenyewe ni neema kubwa, kuweza kuzidiwa na chochote kile bali kule kuuona kwa ukweli ule Uso Mtukufu.”6

Sasa tutawasilisha yale mafundisho ya Ahlul-Bayt (a.s.) kuhusiana na suala tulilolijadili hapo juu.

Madhehebu Ya Ahlul-Bayt (A.S.)

(1) Abdus-Salaam bin Swaleh anasimulia hadithi kupitia kwa Abu al-Swalt al-Hirawi kutoka kwa Imam Ridha (a.s.). Yeye anasema: Nilimuuliza Ali ibn Musa ar-Ridha (a.s.):

“Je, unasemaje kuhusu hili wazo linaloenezwa na watu fulani wa Hadithi kwamba ati waumini watakuja kumtembelea Mola Wao katika makazi yao ya Peponi?”

Imam (a.s.) akajibu akasema:

“Ewe Aba as-Swalt, Mwenyezi Mungu alimbariki Mtume Wake (s.a.w.w.) kwa ubora juu ya viumbe Wake wote, ikiwa ni pamoja na Mitume na Malaika; na ameweka utii wa Mtume (s.a.w.w.) katika uzito ule ule kama utii Kwake Mwenyewe, na kule kumuona Mtume (s.a.w.w.) hapa duniani na kesho akhera kama kumuona Yeye.”

Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur’ani Tukufu:

مَنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ ۚ {80}

“Mwenye kumtii Mtume basi amemtii Mwenyezi Mungu...” (***An- Nisaa; 4: 80***)
Na kisha anasema tena:

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ ۚ {10}

“Bila shaka wale wanaofungamana nawe, basi kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao...” (***Fat’h; 48: 10***)

Na Mtukufu Mtume mwenyewe amesema:

“Yeyote anayenitembelea wakati wa uhai wangu au baada ya kufariki kwangu, anayo malipo ya kumtembelea Mwenyezi Mungu.”

“Cheo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) huko Peponi kitakuwa ndio cha hali ya juu kabisa, na h ii ndio sababu kumuona au kumtembelea yeye kutakuwa ni sawasawa na kumtembelea Mwenyezi Mungu Aliye juu, Mtukufu.”

Abu Swalt akasema:

“Ewe mtoto wa Mtume (s.a.w.w.) tutaitafsiri vipi ile hadithi inayosema: ‘Yeyote anayekiri kwamba hapana mungu ila Allah, atakuja kuuona uso wa Mwenyezi Mungu?’”

Imam (a.s.) akasema:
“Ewe Abu Swalt, yeyote anayehusisha uso kwa Mwenyezi Mungu, anafanya kufuru. Uso huo unaashiria Mitume Wake na Manabii – amani iwe juu yao wote – kwa sababu wanatuongoza sisi kumuelekea Mwenyezi Mungu, Dini Yake, njia Yake na kumtambua Yeye. Hii ndiyo maana yake pale Mwenyezi Mungu anaposema ndani ya Qur’ani Tukufu kwamba:

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ {26}

وَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ {27}

“Kila kitu juu yake kitatoweka. Na itabaki dhati ya Mola Wako, Mwenye utukufu na Heshima.” (***Ar-Rahmaan; 55: 26-27***)

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ ۚ لَهُ الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ {88}

“...Kila kitu kitaangamia isipokuwa uso Wake..(***Qasas; 28: 88***)

Malipo makubwa na ya kupendeza sana juu ya waumini yatakuwa ni kule kukutana na Mitume na Manabii wa Mwenyezi Mungu katika Siku ya Kiyama. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema:

“Wale wanaowachukia Ahlul-Bayt wangu (watu wa nyumbani kwangu) na kizazi changu, hao hawatakutana nami, wala mimi sitakuja kukutana nao katika Siku ya Kiyama.”

Yeye alisema pia wakati akizungumza na masahaba wake:

“Wapo baadhi miongoni mwenu ambao hawataniona mimi kabisa baada ya kuwa wameondokana nami hapa duniani.”

“Ewe Abu Swalt! Mwenyezi Mungu Aliye Juu zaidi haelezewi kwa kumpangia sehemu au nafasi. Wala Yeye hawezi kuzingatiwa kwa kuona au kufikiria!”7

(2) Ibrahim ibn Abu Mahmuud anasimulia kwamba Imam Ridha (a.s.) aliulizwa kuhusu Ayah ifuatayo:

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَاضِرَةٌ {22}

إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ {23}

“Nyuso siku hiyo zitang’aa. Zikingoja malipo kutoka kwa Mola wao. (***Qiyaama; 75: 22–23***)

Yeye (a.s.) akasema:

“Maana yake ni kwamba nyuso zao zitachangamka kwa mng’aro, katika matarajio ya malipo matukufu.”8

(3) Na kuhusu Ayah ifuatayo:

لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۖ {26}

“Na kwa wale waliofanya wema watapata malipo mema na zaidi...”(***Yuunus; 10: 26***)

Tunazo hadithi tatu kutoka kwa Maimamu wa Ahlul–Bayt (a.s.), kila moja ikitoa maelezo yale yale kama hizo nyingine.

(a) Amirul–Mu’minin, Ali ibn Abi Talib (a.s.) amesema:

“Malipo mazuri katika Ayah hii yanahusu Pepo, na hiyo ‘zaidi’ inahusu kurudishwa kwa ziada tena duniani.”

(**b**) Imam al–Baqir (a.s.) amesema:

“Ayah hii inazungumzia kipimo cha nyongeza, ikimaanisha kile ambacho Mwenyezi Mungu atakitoa wakati wa kipindi cha uhai wa duniani; hakitafanyiwa hesabu hiyo Siku ya Hukumu.”
(**c**) Imam Ja’far as–Sadiq (a.s.) amesema:

“ ‘Na zaidi’ itakuwa ni kutoka kwenye duniani hii, kile ambacho kwacho Mwenyezi Mungu

huwaneemesha waumini wakati wa kipindi cha uhai wao na hakipunguzwi kutoka kwenye malipo ya Akhera. Hivyo, Mwenyezi Mungu huwaunganishia wao malipo yote, kwa sababu ya matendo yao mema.”

Inashangaza kwamba wanazuoni kutoka Madhehebu ya Makhalifa wamekuwa siku zote wakichagua kutafsiri Ayah za Qur’ani Tukufu kwa mujibu wa dhana ya Kiyahudi au ya Kikristo kuhusiana na Mungu. Hebu tuchukue mfano wa neno *Nadhirah* ambalo limetafsiriwa na wao kwa maana ya ‘kutazama’.

Raghib ndani ya *Mufradat al-Qur’an* anasema kwamba *Nadhirah* ina maana mbili:

(i) Yule mtazamaji;

(ii) Mtarajia, yule anayesubiria.

Na Qur’ani Tukufu yenyewe imelitumia neno hilo kuashiria “matarajio”. Katika *Suratun-Naml*, Ayah ya 35 tunasoma hivi:

وَإِنِّي مُرْسِلَةٌ إِلَيْهِمْ بِهَدِيَّةٍ فَنَاظِرَةٌ بِمَ يَرْجِعُ الْمُرْسَلُونَ {35}

“Na mimi nitawapelekea zawadi, nami nitangoja watakayorudi nayo wajumbe.” (***An-Naml; 27: 35***)

Ahlul-Bayt (a.s.) wameweka wazi kwamba Ayah hii haizungumzii kumuona Mwenyezi Mungu kwa umbile.

Inatoa maelezo yenye kuonyesha picha ya wazi ya jinsi waumini watakavyochangamka kwa matarajio juu ya malipo yao ya thawabu.

Vivyo hivyo, wakati walipolifafanua hilo neno Ziyada “zaidi” lililotumiwa na Mwenyezi Mungu, wao wameelekeza tafsiri yao juu ya Qur’ani Tukufu yenyewe.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَقِيلَ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا مَاذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ ؟ قَالُوا خَيْرًا ؟ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هَٰذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ ؟ وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ ؟

وَلَنِعْمَ دَارُ الْمُتَّقِينَ {30}

***“Na kwa wale waliofanya wema katika dunia hii* (*pia*) *watapata malipo mema na hakika nyumba ya akhera ni bora zaidi. Na ni bora zaidi makazi ya wachamungu.”* (*An-Nahl; 16: 30*)**

Kutafsiri ‘zaidi’ kama ni kumuona Mwenyezi Mungu ni kitu ambacho kilikuwa hakiaminiki kabisa. Katika mlango ufuatao, ambao ni wa mahitimisho, tutawasilisha ulinganishaji mfupi wa madhehebu hizi mbili, na kuthibitisha hasa kwamba mafundisho halisi kabisa ya Kiislamu, yasiyochafuliwa na kutiwa madoa, yanapatikana kutoka kwa Ahlul-Bayt (A.S.)

Hitmisho

Tawhiid – Kanuni Kuu Na Ya Msingi Ya Ibada Ya Kiislamu.

Mwenyezi Mungu kama anavyofahamika na madhehebu ya Makhalifa:

1. Ana uso wa kibinadamu, na viungo na sehemu!

2. Anakaa juu ya Arsh – Kiti cha Enzi – na mwili Wake unakizidi kikalio cha kiti hicho kwa urefu wa vidole vinne kutoka pande zote!

3. Kiti hicho kimewekwa juu ya mbuzi wa mlimani wanane!

4. Kiti hicho kinanywea na kutoa kelele chini ya uzito wa Mwenyezi Mungu, kama tandiko la farasi jipya, ambalo linatoa makelele chini ya uzito wa mpandaji!

5. Nyakati zingine. Yeye huteremka hadi kwenye mbingu ya chini kabisa na kuwataka viumbe Wake kumuomba na kumsihi!

6. Atakuja kujionyesha Mwenyewe katika Siku ya Kiyama, kwanza katika sura ngeni na halafu kwa uso unaofahamika!

7. Baadhi ya waumini watakuja kumtambua Mola Wao hapo wakat- apoona muundi Wake!

8. Mwenyezi Mungu atakuja kuwatembelea waumini mmoja mmoja kila mtu peke yake, atakutana nao na pia ataongea nao Peponi!

Wanaiita Tawhiid

Ibn Khuzaimah, mwanazuoni mwenye kuongoza katika kundi hili, anakusanya hadithi zinazounga mkono dhana hiyo hapo juu, na anakiita kitabu hicho, *Kitabu cha Tawhiid!*

Bukhari ndani ya *Sahih* yake anao mlango ambamo ndani yake ananukuu na kuzisimulia hadithi hizo zilizotajwa hapo juu na kisha anauita mlango huo *Mlango wa Tawhiid!*

Amefanya vivyo hivyo Muslim ndani ya *Sahih* yake na anauita mlango huo, *Mlango wa Tawhiid!*

Hadithi hizi hasa zinaanzia kwa Abu Huraira na Bwana wake wa Kiyahudi, Ka'b al–Ahbar, na mwaliko wa mawazo ya Kiyahudi juu ya uungu. Kwa hiyo, tunaziainisha hadithi kama hizi kama utomaji maneno kutoka kwenye hadithi za *Israiliyyat*.

Matokeo yake, madhehebu ya Makhalifa inachangia kwenye dhana ya uhusishaji maumbile kwa Mwenyezi Mungu – *anthropomorphic notion* – na kutoa maana halisi, ya neno kwa neno, katika nyingi ya Ayah za Qur'ani Tukufu bila kujali vidokezo vyake vya kiistiari.

Kutoka Madhehebu Ya Ahlul–Bayt (A.S.)

Madhehebu ya Ahlul–Bayt (a.s.) imetufundisha sisi kwamba Mwenyezi Mungu hana anachofanana nacho. Wake Yeye ni Upweke Kamili, na hakuna viungo au sehemu, hakuna nafasi au mipaka inayoweza kuhusishwa Kwake.

Kwa kufanya hivyo, Ahlul–Bayt (a.s.) wametupa sisi maana halisi ya Qur'ani Tukufu na hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuzing'oa zile fikra zote zisizo sahihi ambazo zilipata kupenyezwa kutoka kwenye kambi za Kiyahudi na Kikristo.

Wanazuoni wa Madhehebu hii wamesimulia kutoka kwa Ahlul–Bayt (a.s.), katika vitabu vyao muhimu kama Tafsiir na Kitabu cha Hadithi. Matokeo yake, ule muundo asili wa itikadi ya ya Kiislamu umebakia bila kuchafuliwa.

Sasa ni wazi kabisa kwamba isingekuwa kwa juhudi kubwa na bila kuchoka za Maimamu wa Ahlul–Bayt (a.s.) na wafuasi wao, ile imani kuu ya *Tawhiid* ndani ya Uislamu ingeweza kupotea kabisa, moja kwa moja.

Kinyume na Ahlul–Bayt (a.s.) linakuwepo, ingawa kwa masikitiko sana, kundi la Waislamu ambao wamenasa katika mtego na kuwa mateka kwenye dhana isiyo ya Kiislamu juu ya *Tawhiid*.

Tuna bahati kiasi gani sisi kushikilia kwenye njia ya Ahlul–Bayt (a.s.). Kwa hakika wametuokoa sisi kutokana na ushirikina. Hivyo tunatoa heshima zetu kwao kwa kunukuu kutoka kwenye *Ziyaratul–Jamii'a*.

"Amani juu yenu, enyi Maimam wa Nyumba ya Mtukufu
Mtume, na walinzi wa hazina ya Elimu!

"Amani juu ya viongozi wa kwenye uongovu wa kweli,
na nuru ing'aayo kwenye giza,

"Amani juu ya daraja za utambuzi na ufahamu mtukufu!

"Amani juu ya wale wanaomlilia Mwenyezi Mungu, na wale
ambao ni wasafi katika Tawhiid Yake,

“Mwenyezi Mungu amekuchagueni ninyi kama wasaidizi katika Njia Yake,
wafasiri wa uteremsho Wake, na nguzo imara za Tawhiid Yake,

“Mmewalingania watu kuja kwenye Njia Yake kwa heki– ma na mawaidha mazuri,

“Mwenyezi Mungu aniimarishe, kwa kipindi nitaka– chokuwa hai, katika ufuasi juu yenu,
mapenzi yenu na dini yenu,

“Na aniweke miongoni mwa wale wanaofuata nyayo
zenu, kutembea katika njia yenu na kunufaika kutokana
na mwongozo wenu.”

---

1. Ar–Radd ala al–Jahmiyyah, cha Darami, uk. 53
2. *Tafsiir Tabari – Juz. 11, uk. 73 na 76; na Tafsiir ya Suyuti – Juz. 3, uk.305– 306.
3. Sahih Muslim – uk. 163; Sunan Ibn Majah – Juz. 1, uk. 67; Musnad Ahmad Hanbal – Juz. 4, uk. 332–333; Tafsiir Tabari – Juz. 11, uk. 75; Tafsiir ya Suyuti – Juz. 3, uk. 305.
4. Tafsiir Kabiir – Juz. 17, uk. 78–79
5. as–Durrul–Manthuur – Juz. 6, uk. 292
6. Fi Zilal al–Qur'an cha Sayyid Qutubi – Chapa ya kwanza, Cairo – Juz. 29, uk.208–210
7. Tawhiid, cha Saduuq – uk. 117–118
8. Tawhiid, cha Saduuq – uk. 116

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al–Itrah Foundation:

1. Qur'an Al–Kariim – Tafsir Al–Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na tatu
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu

12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al–Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.

Back Cover

Nafasi Ya Ahlul Bayt Katika Kuhifadhi Mafundisho Ya Uslamu

Madhehebu ya Ahlul–Bayt (a.s.) imetufundisha sisi kwamba Mwenyezi Mungu hana anachofanana nacho. Wake Yeye ni Upweke Kamili, na hakuna viungo au sehemu, hakuna nafasi au mipaka inayoweza kuhusishwa Kwake.
Kwa kufanya hivyo, Ahlul–Bayt (a.s.) wametupa sisi maana halisi ya Qur'ani Tukufu na hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuzing'oa zile fikra zote zisizo sahihi ambazo zilipata kupenyezwa kutoka kwenye kambi za Kiyahudi na Kikristo.

kinyume na Ahlul Bayt (A.S.), hata hivyo, kuna fikra zilizopo za kusiki– tisha za kikundi cha wanachuoni wa Kiislamu ambao wamekuwa mawindo ya dhana ya *Tawhid* isiyo ya Kiislamu. katika kitabu hiki kuna sura mbili zinazo husu *Tawhid,* kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Allamah Askari juu ya somo hili, dhana zote zile zenye kumfananisha Mwenyezi Mungu na mwanadamu kwa uzuri kabisa zimekanushwa.

Wanazuoni wa Madhehebu hii wamesimulia kutoka kwa Ahlul–Bayt (a.s.), katika vitabu vyao muhimu kama Tafsiir na Hadithi. Matokeo yake, ule muundo asili wa itikadi ya ya Kiislamu umebakia bila kuchafuliwa.

Sasa ni wazi kabisa kwamba, kama isingekuwa kwa juhudi kubwa na bila kuchoka za Maimamu wa Ahlul–Bayt (a.s.) na wafuasi wao, ile imani kuu ya *Tawhid* ndani ya Uislamu ingeweza kupotea kabisa

moja kwa moja.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [14]
Tovuti: www.ibn-tv.com [15]

Source URL: https://www.al-islam.org/node/24779

Links
[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/24779%23comment-form
[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/24779%23comment-form
[3] https://www.al-islam.org/person/allamah-syed-murtadha-askari
[4] https://www.al-islam.org/organization/al-itrah-foundation-0
[5] https://www.al-islam.org/person/ramadhani-kanju-shemahimbo
[6] https://www.al-islam.org/library/12-imams
[7] https://www.al-islam.org/library/hadith-collections
[8] https://www.al-islam.org/tags/historia
[9] https://www.al-islam.org/tags/wakristo
[10] https://www.al-islam.org/tags/wayahudi
[11] https://www.al-islam.org/tags/hadithi
[12] https://www.al-islam.org/person/mtume-muhammad-saw
[13] https://www.al-islam.org/person/ahlul-bayt-0
[14] mailto:alitrah@raha.com
[15] http://www.ibn-tv.com